


UKURASA 11

**ZANZIBAR** kujenga shule 25 za ghorofa

UKURASA 5

**RC** Chalamila aingilia kati mgogoro wa Golden Tulip

UKURASA 7



**ISRAEL** yapunguza askari Gaza

UKURASA 19




# Nipashe

Jumatano Januari 3, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581544

www.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper


## ONGEZEKO LA JOTO:

# Wataalamu wahadharisha kiharusi, msongo mawazo

UKURASA 2




## Anayedaiwa kumuua kwa visu mpenzi afariki dunia

UKURASA 3

# Vijana waibua hoja sheria

**KAMATI** Bunge yaita wadau kutoa maoni... *Endelea ukurasa 2 & 4*


**MICHEZO** BENCHIKHA ATAJA GONJWA LINALOTESA MABEKI WA SIMBA UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Mjumbe wa Kamati ya Uongozi wa Baraza la Vyama vya Siasa ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Fedha ya baraza hilo, Salum Mwalimu, akichangia mada katika kikao cha kutathmini maandalizi ya mwisho ya mkutano maalum wa wadau wa demokrasia na vyama vingi vya siasa jana jijini Dar es Salaam. Mkutano huo utafanyika kwa siku mbili kuanzia leo hadi kesho katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC). **PICHA: ORPP**

ONGEZEKO LA JOTO

# Wataalamu: Husababisha kiharusi, msongo wa mawazo

**Na Jenifer Gilla**

ONGEZEKO la joto katika mikoa ya pwani limeanza kuleta athari kiafya kwa wakazi wa maeneo hayo huku wataalamu wakitahadharisha linaweza kuleta kiharusi cha joto na msongo wa mawazo.

Taarifa iliyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) jana ilitaja mikoa ya Dar es Salaam na Zanzibar kuwa na kiwango cha juu cha joto cha nyuzi 33, ikifuatiwa na Tanga (32) na Dodoma (29).

Athari zilizoanza kujitokeza ni baadhi ya watu kutokwa na vipele vidogo mwilini ambavyo baadaye husababisha vidonda kutokana na kujikuna hasa kwa watoto.

Joto hilo pia husababisha watu kujisikia kuchoka kama anavyoeleza mkazi wa Vingunguti, jijini Dar es Salaam, Leonard James kuwa linamfanya kukosa usingizi wa kutosha usiku na kuathiri utendaji kazi wake kutokana na kuchoka na kusinzia.

Alisema kwa wiki mbili tangu hali hiyo ilipoanza analazimika kukaa macho saa sita usiku akihangaika kupata unafuu.

"Sio siri joto la safari hii ni kiboko na limekuja mapema, ikifika saa tisa usiku unaamka na kukaa kwa sababu hata feni hazifanyi kazi, unaona zinasambaza joto tu huko ndani," alisema.

Elizabeth Charles, mkazi wa Buza amelalamika watoto wake wanavyoathirika kwa kushindwa kuvumilia hali hiyo na kulia usiku kucha, akilazimika kukesha kuwapepea.

Alisema joto limewasababishia vipele vinavyowafanya wajikune na hatimaye kutoka vidonda hali inayowakosesha raha ya kucheza na wenzao.

Wakazi wa maeneo ya Kinondoni, akiwamo Salma Katalawanda, kwa sasa wanalazimika kulala nje na familia zao kutafuta afueni ya upepo.

**WATAALAM WANAZUNGUMZIAJE**

Daktari wa Binadamu kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini ya KCMC, Dk. Norman Jonas, anasema kwa kawaida mwili wa mwanadamu umeundwa na mifumo mbalimbali ya kurekebisha joto la ndani lisipande kupita kiasi na linapozidi mifumo hiyo inatoa jasho mwilini ili kujipoza.

Anasema joto linapozidi kuwa kali mwili unaweza kuelemewa na joto la mwili kupanda kupita kiasi na husababisha mtu kupoteza maji mengi, madini chumvi muhimu na kuathiri utendaji kazi wa mifumo muhimu kama ufanyaji kazi wa vichocheo vya mwili.

Alisema madhara yake ni misuli kukaza kwa baadhi ya watu hasa wenye misuli mikubwa kama ya miguu na huambatana na maumivu makali.

Pia, husababisha mwili kuelemewa na hali joto ambayo huambatana na viashiria kama vile kiu kali, mwili kuwa dhaifu, maumivu ya kichwa, kichefuchefu, tumbo kuuma, ngozi kunata au kukauka pia hisia za vitu kuchomachoma kwenye ngozi na upele.

Alisema joto likiwa kali katika mwili wa binadamu na lisipodhibitiwa kwa wakati linaweza kusababisha ugonjwa ujulikanao kama wa kiharusi cha joto.

Alisema hali hiyo huja na dalili mbalimbali ikiwamo moyo kwenda mbio na kupumua haraka, ngozi kuvilia na kwa wenye ngozi nyeupe huonekana nyekundu, kuhisi kichefuchefu na kutapika.

"Iwapo mwili ukishindwa kupoa baadhi hupata dalili za kuchanganyikiwa, kupoteza fahamu au kupata degedege," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Jonas, japokuwa joto huathiri watu wote, lakini kuna makundi yanaathirika zaidi kama vile watoto, wazee, na wenye magonjwa ya kudumu.

"Joto kali huweza kuathiri hata kijana mwenye afya iwapo amefanya kazi ngumu au mazoezi muda mrefu bila kupumzika au kujipoza," alisema.

Daktari Bingwa wa Tiba ya Familia kutoka hospitali ya Agakhan, Willbroad Kyejo, alisema joto kali pia huwaletea madhara watu wenye matatizo ya mfumo wa upumuaji kama vile pumu kwa kuwa hewa inakuwa nzito.

Alisema pia hali hiyo kusababisha mwili kuchoka au kuishiwa nguvu na mtu kushindwa kufanya majukumu yake kwa kuwa inasababisha kupoteza hamu kufanya kazi.

Mtaalam wa Saikolojia, Dismas Lyassa alisema joto pia husababisha msongo wa mawazo na uwezo wa kufikiri kupungua na kumwondolea hamu ya kufanya kazi.

**NAMNA YA KUJIKINGA**

Dk. Jonas anashauri mtu anapoona dalili za mwili kuanza kuzidiwa na joto kali achukue hatua za kupoza kama kupumzika sehemu yenye ubaridi au kivuli, kutoa nguo za ziada mwilini, kunywa maji au vinywaji vya kuongeza maji mwilini.

"Iwapo hali ni mbaya zaidi inaambatana na misuli kukakamaa ongeza na chumvi kiasi kijiko cha chai katika lita moja ya maji kisha unywe," alifafanua.

Alishauri kwa wenye dalili za kiharusi cha joto huhitaji huduma ya haraka kwa kuwa ikiachwa bila kutibiwa wanaweza kupata madhara makubwa hata kifo.

Dk. Wilbroad alishauri watu kuvaa nguo nyepesi hasa zenye rangi nyeupe na kuepuka nzito zenye rangi nyeusi ambazo hunyonya joto na kufanya mwili upate joto haraka.

Alisema pia ni muhimu mazingira ya ndani ya nyumba kuwa na mzunguko mzuri wa hewa na kuwa na vifaa vya kupoza joto kama kiyoyozi au feni.

Alishauri wanaokunywa pombe kupita kiasi kuchukua tahadhari katika msimu huu kwa sababu kemikali ya pombe husababisha mwili kupoteza maji mengi.

Pia, wenye matatizo ya upumuaji wanashauriwa kukaa kwenye maeneo yenye kivuli au hewa ya kutosha kwa kuwa joto kali huweza kuchochea kuzidiwa.

Alishauri wazazi wanapotoka na watoto kubeba maji ya kunywa ya kutosha, kuwavalisha kofia na nguo nyepesi zinazoachia mwili na kuepuka kuwafungia ndani ya gari kunaweza kusababisha kifo kwa haraka kutokana na shambulio la joto kali.

# Vijana upinzani waibua hoja miswada sheria

**Na Halfani Chusi**

VIONGOZI wa Jumuiya ya Vijana kutoka vyama vya upinzani nchini, wametoa mapendekezo 16 kuhusu miswada ya sheria, ikiwamo minne ya masuala ya uchaguzi.

Viongozi hao ni kutoka ACT-Wazalendo, Chama cha Wananchi (CUF) na NCCR-Mageuzi ambao kwa pamoja wametoa mapendekezo kuhusu Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2023 na Muswada wa Sheria ya Tume ya Uchaguzi wa Mwaka 2023.

Mingine ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba Tano wa Mwaka 2023 na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa Mwaka 2023.

Miswada hiyo iliwasilishwa na kusomwa na serikali kwa mara ya kwanza bungeni Novemba 10, mwaka jana.

Viongozi hao kwa pamoja kwenye taarifa yao waliyoitoa kwa vyombo vya habari jana jijini Dar es Salaam, walisema miswada hiyo haijabeba hoja zenye ustawi kwa vijana huku wakitoa mapendekezo hayo.

Akizungumza kwa niaba ya viongozi wengine, Katibu Mkuu wa Vijana wa CUF, Iddi Mkanza, alisema wamebaini kuwa vifungu vingi vya miswada hiyo vimekinzana na Katiba na kwamba hali hiyo haitaleta usawa na haki nchini, haitaimarisha demokrasia na kupanua ushiriki wa kisiasa kwa wananchi vijana na makundi mengine.

Mkanza pia alisema miswada hiyo haitaleta uwajibikaji kwa viongozi sababu ya kutokuwa na chaguzi huru na haki.

**MAPENDEKEZO**

Kutokana na kasoro hizo, alisema wanapendekeza kuondolewa kwa kifungu cha 6(1) na 6(2) katika Muswada wa Sheria ya Uchaguzi kinachohusu kuwatumia wakurugenzi wa halmashauri na watumishi wa umma kusimamia uchaguzi.

Alisema Kifungu cha 18(2) kinapaswa kurekebishwa, muundo wa Tume ya Uchaguzi ugawanywe katika sehemu mbili, yaani bodi na menejimenti, kwamba bodi iwe chini ya Mwenyekiti wa Tume na iajiri mkurugenzi wa uchaguzi kwa sifa zitakazo ainishwa na kwa uwazi.

Kadhalika, alipendekeza Kifungu cha 9(3) kifutwe kumwondoa Mkurugenzi wa Uchaguzi kuwa Katibu wa Kamati ya Usaili na badala yake Katibu wa Kamati ya Usaili awe Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Alisema sifa za wajumbe wa tume katika Kifungu cha 7(2) cha Muswada wa Sheria Mpya ya Tume ya Uchaguzi, uzingatie vijana na kwamba kifungu kitamke angalau wajumbe wawili kati ya watano wawe vijana.

Alisema vifungu vya 35(1)(2) na 51(1) katika Muswada wa Sheria ya Uchaguzi vifutwe sababu viko kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 Ibara ya 21(1)(2) inayoruhusu uhuru wa mtu kushiriki katika masuala ya kiuongozi na uamuzi.

Pendekezo lingine ni kufanyike kwa marekebisho katika Muswada wa Sheria ya Uchaguzi Kifungu cha 85(1) na 14(1), kiruhusu wananchi kupiga kura ya udiwani, ubunge na urais popote walipo hata kama ni tofauti na maeneo waliyojiandikishia, kwamba suala hilo linawezekana kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Alisema Muswada wa Sheria ya Uchaguzi ujumuishe pia uchaguzi wa serikali ya mtaa na uitwe Muswada wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge, Madiwani na Viongozi wa Serikali ya Mitaa, Vijiji na Vitongoji.

Kifungu cha 10(1)C cha Muswada wa Sheria ya Uchaguzi, alisema kinachozuia wafungwa kupiga kura kinapaswa kufutwa sababu kina kinzana na Ibara ya 5(1) ya Katiba, pia kina kinzana na hukumu ya Mahakama Kuu katika kesi No.3 ya 2022 ya Tito Magoti.

Kadhalika, walipendekeza kwamba fedha za kuendesha shughuli za NEC zitoke kwenye mfuko mkuu wa serikali ili kuongeza uhuru na ufanisi wa tume katika kutekeleza majukumu yake tofauti na sasa hivi ambapo NEC inatengewa na kupewa fedha kama hisani kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu.

Pendekezo lingine ni kuondoa mamlaka za serikali (Msajili wa Vyama vya Siasa na Mwanasheria Mkuu wa serikali) katika kuweka mapingamizi dhidi ya wagombea.

Pia kifungu kiruhusu mtu yeyote kuweka pingamizi na siyo Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa au Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

HABARI KITAIFA

# Aliyebabuka ngozi kwa dawa apoteza maisha

**Na Rama Suleiman,** ZANZIBAR

HALIMA Oma Ali (29) aliyekuwa akipatiwa matibabu ya kubabuka ngozi katika Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja, amefariki dunia.

Halima ambaye alihamishiwa Mnazi Mmoja Desemba 27, mwaka jana, akitokea Hospitali ya Abdalla Mzee, mkoani Pemba, alikuwa akitibiwa ugonjwa ambao kitabibu unaitwa TEN ambao ulisababishwa na madhara aliyopata kutokana na dawa alizopewa hospitalini.

Aliaga dunia juzi saa 11:00 jioni wakati akiendelea kupatiwa matibabu na kuzikwa katika makaburi ya Mwanakwereke siku hiyo hiyo majira ya usiku.

Kwa mujibu wa daktari bingwa wa maradhi ya ngozi, Dk. Salama Makame, Halima alipatwa na madhara makubwa mwilini mwake baada ya kutumia dawa ya Carbamezapine (CPZ) aliyopewa wakati akipatiwa matibabu kisiwani Pemba.

Kabla ya kufikishwa Mnazi Mmoja, alianza matibabu katika Hospitali ya Micheweni na baada ya kupata madhara hayo Desemba 19 na hali ilipozidi kuwa mbaya kwa sababu ngozi ya kubabuka na kufanya vidonda mwili mzima, ndipo alipata rufani Hospitali ya Abdalla Mzee Mkoani kwa ajili ya matibabu zaidi.

Nipashe ilifika nyumbani kwa marehemu kulikofanyika msiba eneo la Melitano, Jimbo la Kijito Upele, Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.

Mama wa marehemu, Maryam Khamis Hamad, alisema kabla ya mauti haujamfika hali yake kiafya iliimarika tofauti na siku zote alipokuwa amelazwa hospitalini hapo.

"Tunawashukuru madaktari wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kupambania kuokoa maisha ya mtoto wetu lakini ilishindikana na siku ambayo anafariki dunia asubuhi yake. Hali yake ilikuwa nzuri kidogo na ikatupa matumaini kwamba angepona lakini ndiyo kazi ya Mwenyezi Mungu haina makosa," alisema mama huyo huku akitiririkwa na machozi.

Aidha, alisema kabla ya kufariki dunia, aliomba azungumze na watoto wake walioko Pemba kwa njia ya simu na alizungumza na mtoto wake wa kwanza wa kike mwenye umri wa miaka saba huku akimhimiza kusoma kwa bidii.

"Nalikumbuka neno lake la mwisho kabla ya kufa akiwa hospitali aliniambia mama msihangaike kwa ajili yangu na nikifa naomba msinililie maana Mwenyezi Mungu ndiye kashaandika," alinukuu maneno hayo ya marehemu kabla ya kukata roho.

Alisema ilipofika majira ya saa 10:00 jioni, hali ilianza kubadilika na kutozungumza chochote hadi mauti yalipomkuta huku madaktari wakiendelea kumpatia matibabu.

"Madaktari walijitahidi na tumeridhishwa na huduma alizopata mtoto wetu maana ilifika hatua vidonda alivyokuwa navyo mwili vikawa vimeanza kukauka tofauti na ilivyokuwa mwanzo alipofikisha Desemba 27, mwaka jana," alisema.

Mume wa marehemu, Idrisa Shindano, alisema alipewa taarifa ya kifo cha mke wake saa 12:00 jioni ya siku aliyofariki dunia akiwa baharini katika shughuli zake za uvuvi na alishindwa kumzika mke wake kutokana na umbali aliokuwapo baharini na hali ya hewa ilikuwa mbaya baharini.

"Nilitamani nimzike kwa mikono yangu mke wangu lakini imeshindikana. Nimefika hapa usiku mkubwa wakati mke wangu tayari ameshazikwa katika makaburi ya Mwanakwerekwe," alisema Shindano.




Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, akitoa salama za pole kwa familia ya Mzee William baada ya kuondokewa na binti yao, Rechal William (19), aliyefariki dunia katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama kwa kukosa huduma Desemba 27, mwaka jana katika ibada ya maziko Mtaa wa Mji Mwema, Kata ya Mhongolo juzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Mtuhumiwa aliyemuua mpenzi wake kwa kumchoma visu afariki

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

LICHA ya kufeli jaribio la kwanza la kutaka kukatisha uhai wake kwa sumu ili kukwepa tuhuma za shambulio la mauaji ya mpenzi wake, Beatrice Minja, anayedaiwa kumchoma visu 25, mtuhumiwa Lucas Tarimo, naye amefariki dunia ndani ya saa 48 akiwa chini ya ulinzi wa polisi.

Beatrice (47), mfanyabiashara wa Tarakea, Rombo mkoani Kilimanjaro, alipoteza maisha wakati akitetea uhai wake katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC iliyoko Moshi, Desemba 27, mwaka jana.

Jana Daktari Mfawidhi wa Hospitali Teule ya Huruma inayomilikiwa na Kanisa Katoliki Jimbo la Moshi kwa ubia na serikali, Daria Mushi, alithibitisha kuwa Tarimo alifariki dunia wakati akiendelea kupatiwa matibabu.

"Ni kweli Tarimo amefariki jana usiku wakati akiendelea kupatiwa matibabu," alisema Dk. Mushi.

Novemba 12, mwaka jana, mtuhumiwa huyo alidaiwa kumshambulia Beatrice kwa kisu sehemu mbalimbali za mwili na baadaye alipelekwa katika Hospitali ya KCMC, ambako alikaa kwa siku 47 kisha kupoteza maisha, Desemba 27.

Kwa mujibu wa Msemaji wa Jeshi la Polisi, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) David Misime, Tarimo alimakatwa Desemba 31, 2023 majira ya alfajiri akiwa amejificha katika Kijiji cha Jema, Oldonyosambu, Ngorongoro mkoani Arusha, akijiandaa kukimbilia nchi jirani.

Taarifa ya jeshi hilo ilieleza kuwa mtuhumiwa baada ya kuona mkono wa serikali unamfikia, alikunywa sumu inayotumika kuua wadudu na alipatiwa huduma ya kwanza ili taratibu zingine za kisheria ziendelee.

Alipotafutwa kuzungumzia tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP) Simon Maigwa, alisema mtuhumiwa huyo alifariki dunia saa 7:17 usiku wa kuamkia jana.

"Hakuna ubishi, ni kweli mtuhumiwa (Tarimo) amefariki dunia. Kama utakumbuka Tarimo alikunywa sumu aina ya 'Dudu Will' na Wasonjo walipogundua amekunywa hiyo sumu, walimtapisha kwa kumpa maziwa na baadaye walimpeleka Zahanati ya Jema huko Ngorongoro.

"Polisi waliojulishwa na Wasonjo (jamii ya wafugaji) walikwenda kumkamata na kumshikilia na alipoletwa Kilimanjaro, alipelekwa wilaya husika (Rombo) na kupelekwa hospitalini kuendelea na matibabu.

"Baada ya kumfikisha Hospitali ya Huruma, tulimfungulia jalada la kwanza la kesi ya kutaka kujaribu kujiua ili kukwepa kujibu tuhuma za mauaji ya mpenzi wake. Na jalada la pili, ambalo tulikuwa tunaandaa lilikuwa ni la mauaji ya kukusudia ya Beatrice Minja, lakini ndiyo hivyo kazi imeisha hivyo," alisema Kamanda Maigwa.




Msemaji wa Kampuni ya Tumbaku Alliance One, Wakili John Magoti (kulia), akimkabidhi fulana Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang', Francis Namaumbo, ikiwa sehemu ya msaada wa bidhaa mbalimbali walizotoa zenye thamani ya Sh. milioni 25 kwa ajili ya waathirika wa maporomoko yaliyotokea wilayani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Heche ahojiwa taarifa ya polisi kuteka kijana

**Na Timoth Itembe,**
TARIME

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Heche ameitwa na kuhojiwa katika Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi (RCO) Mkoa wa Mara kwa muda wa saa kadhaa kisha kuruhusiwa kuendelea na shughuli zake.

Heche ambaye pia ni Mbunge wa zamani wa Tarime Vijijini, aliitwa kituoni hapo jana kwa ajili ya kuhojiwa juu ya taarifa aliyoitoa katika mtandao wake wa X ikilituhumu jeshi hilo kumteka kijana aliyejulikana kwa jina moja la Sele katika maeneo ya Serengeti.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu baada ya kuhojiwa kituoni hapo, Heche alisema alipokea wito wa kufika katika ofisi za Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara Desemba 19, 2023 kwa ajili ya kujibu madai hayo aliyoyachapisha mtandaoni.

"Nimeitwa Musoma nikahojiwa kuhusu nilichokiandika kutokana na kijana Sele, mkazi wa Masanga wilayani Tarime kupotea katika mazingira ya kutatanisha huko wilayani Serengeti ambaye alichukuliwa na watu waliojitambulisha kuwa ni askari polisi," alisema Heche.

Alisema baada ya muda pikipiki ya kijana huyo ilionekana katika kituo cha polisi kabla ya kutolewa katika mazingira ya kutatanisha na kijana huyo aliyechukuliwa mchana mpaka jana alikuwa hajulikani aliko.

"Nimeeleza ninachokifahamu juu ya upotevu wa kijana huyo mikononi mwa jeshi lenye jukumu la kulinda raia na mali zao kwani hatuwezi kuvumilia kuona watu wanapotea tu na sisi tukakaa kimya," alisisitiza Heche.

Awali Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, Salum Morcase, alithibitisha kuitwa kwa kiongozi huyo wa CHADEMA na kueleza kuwa wito huo ni kwa ajili ya tuhuma alizozitoa dhidi ya Jeshi la Polisi.

"Kuna taarifa alizitoa kuhusu polisi Serengeti, hivyo ameitwa kwa ajili ya kuhojiwa juu ya tuhuma hizo tu hakuna kingine," alisema Morcase.

# Kamati ya Bunge leo kuanza kuchambua miswada

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria leo imeanza vikao vyake vya kuchambua na kupokea maoni ya wadau ya miswada ya sheria ikiwamo minne ya masuala ya siasa na uchaguzi.

Novemba 10, 2023 miswada hiyo ilisomwa bungeni kwa mara ya kwanza na kupelekwa kwenye kamati hiyo kwa mujibu wa Kanuni ya 97(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili kufanyiwa uchambuzi na kupokea maoni ya wadau.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Bunge Desemba 30, 2023, miswada hiyo ni wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023, Sheria ya Tume ya Uchaguzi wa mwaka 2023, Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali namba tano wa mwaka 2023 na Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa wa mwaka 2023.

Katibu wa Bunge alitangaza kamati hiyo kuwaalika wadau kutoa maoni kuhusu miswada hiyo kuanzia Januari 6, 8 hadi 10, mwaka huu katika Ofisi ya Bunge, jijini Dodoma.

Miongoni mwa yaliyomo kwenye miswada hiyo ni pamoja na muundo mpya wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) utakaokua na kamati maalum itakayosaili wajumbe na Mkurugenzi wa Uchaguzi.

Aidha, inapendekezwa kufutwa kwa utaratibu wa kupita bila kupingwa kwa mgombea na badala yake atapigiwa kura ya ndiyo au hapana na atakuwa amechaguliwa kihalali kuwa mbunge endapo atapata kura nyingi za ndiyo kati ya kura zote halali zilizopigwa.

Pia, inapendekezwa kila chama cha siasa kuwa na sera ya jinsia na ujumuishi wa makundi maalum na maandamano ya vyama vya siasa yatafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi na umeainishwa utaratibu wa kuzingatiwa kabla na wakati wa kufanya maandamano au mikutano.

Katika Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023 unasema Kamati ya Usaili itapokea na kufanya uchambuzi wa maombi ya watu wanaoomba kuteuliwa kuwa wajumbe wa tume hiyo na kupendekeza majina ya watu wenye sifa kwa Rais kwa ajili ya uteuzi na mjumbe atatumikia nafasi hiyo kwa miaka mitano.

Inapendekezwa kuwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi watateuliwa na Rais kwa kuzingatia masharti yaliyopo katika Ibara ya 74 ya Katiba na watapaswa kuwa Majaji wa Mahakama Kuu au ya Rufani au kuwa na sifa ya kuwa Wakili na amekuwa na sifa hizo kwa zaidi ya miaka 15.

Pia, Sheria inayopendekezwa inaweka utaratibu wa Rais kuunda kamati ya uchunguzi endapo anaona inafaa, ambayo itafanya uchunguzi na kumshauri ipasavyo kuhusu kuondolewa kwa mjumbe wa tume hiyo ya uchaguzi.

**TUME KUWA CHOMBO HURU**

Inapendekezwa Tume itakuwa chombo huru na kinachojitegemea na maamuzi yake hayataingiliwa na chombo chochote au kulazimika kufuata maagizo ya mtu yeyote au Idara yoyote ya serikali au maoni ya chama chochote cha siasa.

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

Kama sheria hiyo itapitishwa na Bunge, kutakuwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi atakayeteuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume na atakuwa na sifa ya kuwa raia wa Tanzania wa kuzaliwa, mtumishi wa umma mwandamizi, mwaminifu na mwadilifu na ambaye hajawahi kushika nafasi ya madaraka ya juu katika chama chochote cha siasa.

Pia, inaweka masharti kwamba mtu yeyote atakayekuwa anatekeleza majukumu ya Tume atachukuliwa kuwa mtumishi wa tume hiyo kwa kipindi chote atakachokuwa anatekeleza majukumu hayo na atapaswa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni za utekelezaji wa majukumu yake.

**GHARAMA ZA UCHAGUZI**

Kadhalika, katika muswada wa sheria ya gharama za uchaguzi, inapendekeza kuondolewa sharti la vyama vya siasa kuwasilisha stakabadhi halisi za matumizi ya gharama za uchaguzi kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ili stakabadhi hizo zibaki kwenye vyama kwa ajili ya kuwasilishwa kwa mkaguzi.

Kwenye marekebisho hayo, kumewekwa adhabu chama cha siasa kitakachomruhusu asiye raia wa Tanzania kushiriki katika mchakato wa kufanya maamuzi ndani ya chama husika. Lengo ni kukomesha vitendo vya wasio raia kuingilia katika maamuzi ya vyama vya siasa kwa kuwa sasa sheria inaweka katazo bila adhabu.

Pia, inapendekezwa kuondolewa kwa takwa la wagombea kuwasilisha taarifa kuhusu timu ya kampeni kwa Mkurugenzi wa halmashauri, Katibu Tawala wa wilaya na Ofisa Mtendaji kata na badala yake ziwasilishwe kwa Msimamizi wa Uchaguzi na Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi.

Marekebisho mengine ni kuboreshwa utaratibu wa kuchukua na kuwasilisha fomu za tamko la gharama za uchaguzi ili fomu zichukuliwe kwa msimamizi wa uchaguzi wakati mtia nia anachukua fomu za kuomba uteuzi na kuuasilishwa wakati wa kurejeshwa fomu za uteuzi. Lengo ni kutoa muda wa kutosha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kupitia taarifa zinazowasilishwa na watia nia kuhusu gharama wanazokusudia kutumia katika uchaguzi kabla hawajaanza shughuli za kampeni.

**MKUTANO MKUU WA CHAMA**

Katika mabadiliko ya sheria ya vyama vya siasa, inapendekezwa katika mkutano mkuu wa chama cha siasa sasa kitawezeshwa kukasimisha jukumu lake la kuteua mgombea urais wa Zanzibar na lengo ni uteuzi wa mgombea huyo kufanywa na Halmashauri Kuu ya chama.

Kwenye muswada huo, vyama vya siasa vinaruhusiwa kushirikiana hata wakati wa uchaguzi mdogo kwa kuzingatia masharti yaliyomo katika sheria na kumeongezwa takwa kwa chama cha siasa kuwasilisha nakala ya kanuni zake wakati wa maombi ya usajili wa muda na kumewekwa kifungu cha kukinyima sifa chama cha siasa ya kusajiliwa endapo Katiba na kanuni zake zinaruhusu matumizi ya lugha inayoweza kuhatarisha usalama wa nchi.

**SHERIA MOJA YA UCHAGUZI**

Inapendekezwa kutungwa kwa sheria ya uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2023 ambayo inakusudia kuunganisha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa.

Hatua hiyo inalenga kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa masharti yote ya sheria hizo ambazo hutekelezwa na mamlaka moja ambayo ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

HABARI KITAIFA

# Zanzibar kujenga shule 25 za ghorofa

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid, amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imedhamiria kujenga shule 25 za ghorofa katika mwaka wa fedha 2023/24 ili kuboresha sekta ya elimu.

Maulid alisema hayo jana katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi katika Shule ya Msingi ya Mwambe katika shamrashamra za maadhimsho ya Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema ujenzi wa shule hizo ni sehemu ya ahadi za serikali ya awamu ya nane inayoongozwa na Dk. Hussein Ali Mwinyi katika kuwaletea wananchi maendeleo ya elimu.

Spika Maulid aliwataka wananchi wa Mwambe, Wilaya ya Mkoani kisiwani Pemba, kuyaenzi na kuyalinda Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwa ndiyo mkombozi wa upatikanaji wa huduma mbalimbali ikiwamo elimu.

Alisema kabla ya Mapinduzi, watawala walitoa huduma hizo kwa matabaka na kuwafanya watoto wa wanyonge kukosa huduma mbalimbali kama elimu na matibabu.

Madhila hayo na mengine, alisema ndiyo yaliyowafanya waasisi wa Mapinduzi kufanya kila juhudi kuuondoa utawala uliokuwapo, ili kuwarejeshea heshima wazalendo.

"Leo tukiwa ndani ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar, wananchi wa Mwambe na maeneo mingine, tunayo kila sababu ya kuyalinda, kuyaenzi Mapinduzi hayo, maana ndiyo ambayo sasa matunda yake tunayatumia," alisema.

Kuhusu uwapo wa shule hiyo ya ghorofa mbili, aliwataka wananchi na walimu, kushirikiana ili itoe wataalamu wa fani mbalimbali kwa maendeleo ya taifa.

Alisema serikali imetumia fedha nyingi katika ujenzi wa shule hiyo, hivyo ili matunda yake yaonekane, hakuna budi kuongeza ufaulu ambao utasababisha upatikanaji wa wataalamu wa baadaye.

Kumalizika kwa ujenzi wa shule hiyo mwanzoni mwa mwaka ujao, alisema utaondoa moja kwa moja mikondo mitatu ambayo awali ilikuwa katika maeneo hayo ya Mwambe.

"Naelezwa kuwa ndani ya miaka hii mitatu ya uongozi wa Dk. Mwinyi, sambamba na Miaka 60 ya Mapinduzi, ndani ya jimbo hili la Kiwani, tumeshajenga



skuli (shule) tatu za ghorofa, zikiwamo za Mwambe na Kiwani," alisema.

Spika Maulid aliwataka wananchi wa Mwambe kuitunza shule hiyo mara itakapomalizika, ili kutumiwa na vizazi vijavyo.

Awali Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Mwanakhamis Adam Ameir, alisema ujenzi wa shule hiyo ni moja ya mikakati ya serikali katika kuweka elimu kipaumbele cha pekee.

Alisema tangu serikali ya awamu ya nane ilipoingia madarakani, iliweka mikakati ya kuimarisha miundombinu ya elimu, ikiwamo ujenzi wa shule za ghorofa, ili kupunguza msongamano wa wanafunzi.

Naibu Katibu Mkuu alisema ujenzi wa shule kama hizo una mawanda mapana ya kuondoa mikondo miwili kwa shule zote za Unguja na Pemba ili kuwapa walimu nafasi nzuri zaidi za kufundisha.

"Kwa mfano hapa Mwambe, tulikuwa na mikondo mitatu, lakini mwanzoni mwaka huu, tulishafungua skuli moja ya ghorofa na leo tunaweka jiwe la msingi skuli hii iliyopo Chanjaani. Haya yote lengo ni kuona wanafunzi wanapata muda wa kujifunza," alisema.

Eneo la Mwambe, alisema kwa sasa lina shule tatu za msingi ambazo zina jumla ya wanafunzi wa msingi na maandalizi 4,658, wakiwa na vyumba 68 vya kusomea.

Naye Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdull-ghulam Hussein, alisema ujenzi wa skuli hiyo ni utekelezaji wa vitendo wa maana ya Mapinduzi daima.

Alieleza Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi wakati akilihutubia Baraza la Wawakilishi, alieleza kutotaka hadithi ya Mapinduzi, bali sasa ni kuwaonyesha wananchi matunda yake.

Mapema, Mkuu wa Wilaya ya Mkoani, Khatib Juma Mjaja, alisema Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964, yalifanyika ili kuwakomboa wananchi na kupata haki zao. Alisema ndani ya miaka 60, watoto wa kinyonge wanapata haki ya elimu, matibabu, maji safi na salama na hata miundombinu ya barabara.

Ujenzi wa shule hiyo ya ghorofa, ulianza Mei, 2023 na unatarajiwa kukamilika mwanzoni baadaye mwezi huu na inajengwa na Kampuni ya Mwinyi Building na kusimamiwa na Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) na sasa umefikia asilimia 60.

## Wawili wauawa mkesha wa mwaka mpya

**Na Samson Chacha,** TARIME

WATU wawili wakazi wa Tarime mkoani Mara, wameuawa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali na mwingine kukatwa mapanga.

Waliouawa katika matukio hayo ni dereva wa lori la mchanga, Joseph Sabai mkazi wa Mjini, Kata ya Nyamongo na Alex Mandaki mkazi wa Mtaa wa Starehe, Kata ya Nyamisangura, Tarime mjini.

Diwani wa Nyamisangura, Thobias Ghati na Mwenmyekiti wa Mtaa wa Starehe, Mwita Meck na mama wa marehemu, Bertha Werema, walisema tukio hilo la kusikitisha la mauaji ya kijana Alex Mandaki lilitokea usiku wa mkesha wa mwaka mpya wa 2024 katika mtaa wa Mwangaza.

Mandaki akiwa na wadogo zake wawili, walikuwa wakirejea nyumbani kutoka matembezini ndipo walipokutana na vijana waliokuwa na mapanga wakimfukuza binti mmoja aliyefahamika kwa jina la Lydia naye akakimbilia kwa kina Alex kutaka kupata msaada ili kujiokoa kutoka mikono ya vijana hao waliokuwa na mapanga.

Viongozi hao na mama mzazi wa marehemu walisema vijana hao watatu waliokuwa na mapanga, walimvamia Mandaki na kuanza kumkata mapanga mikononi huku akipiga kelele na wadogo zake kuomba msaada kutoka kwa majirani.

Baada ya kutekeleza uhalifu huo, Ghati alisema vijana hao walitoroka kuelekea mtaa wa Ronsoti na watu walijitokeza na kumchukua Mandaki kumpeleka Hospitali ya Wilaya lakini alipoteza maisha kabla ya kupatiwa matibabu kutokana na kutokwa damu nyingi.

"Tunashukuru Lydia aliwatambua vijana hao waliofanya mauaji hayo ya Mandaki. Tunatoa wito kwa wananchi kutoa ushirikiano kuwakamata wahusika wote wa mauaji ya kijana huyo pia kuwafichua wahalifu wengine ili kukamatwa na kufikishwa katika mkono wa sheria," alisema Diwani Ghati.

Katika tukio lingine usiku huo wa mkesha wa mwaka mpya,

Mkazi wa Kijiji cha Mjini Kati, Nyamongo, Kata ya Matongo, Joseph Sabai, dereva wa lori la mchanga, alichomwa na kitu chenye ncha kali shingoni na kufariki dunia baada ya damu kuingia tumboni na kuchelewa kupatiwa matibabu haraka.

Kutokana na mauaji hayo, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wananchi, liliendesha msako usiku huo nyumba kwa nyumba na kumkamata mtuhumiwa Sugurya Kerongo.

Diwani wa Matongo, Godfrey Kegoye, alisema wamesikitishwa na tukio hilo lakini wanawapongeza wananchi na polisi kwa kufanya msako ambao ulifanikisha kukamatwa kwa mtuhumiwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Tarime Rorya, Kamishna Msaidizi (ACP) Michael Njera, alithibitisha jana kutokea kwa matukio hayo mawili ya mauaji.

Alisisitiza kuwa polisi pamoja na kumshikilia mtuhumiwa Sungurya, wanaendelea na msako wa wananchi kutoa ushirikiano ili kukamatwa kwa watuhumiwa hao wengine.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Kongole TRA kuvuka lengo, juhudi zaidi zinahitajika

**MAMLAKA** ya Mapato Tanzania (TRA), juzi ilitangaza makusanyo ya mapato katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha wa 2023/24, yakionyesha kupanda kwa asilimia 11.5 kulinganisha na kiasi kilichokusanywa kwa kipindi kama hicho kwa mwaka wa 2022/23.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata, katika kipindi hicho cha Julai hadi Desemba 2023, mamlaka imekusanya Sh. trilioni 13.92 ya malengo ambayo ni sawa na asilimia 97.98. TRA katika malengo yake kwa kipindi hicho ilipanga kukusanya Sh. trilioni 14.21 katika mwaka wa fedha wa 2022/23, katika kipindi kama hicho, mamlaka hiyo ilikusanya Sh. trilioni 12.49.

Licha ya kuweka rekodi hiyo, TRA iliweka rekodi mpya ya kiwango cha makusanyo kwa mwezi tangu kuanzishwa kwake kwa kukusanya Sh. trilioni 3.05 ikiwa ni ufanisi wa takriban asilimia 103. Katika kipindi hicho cha mwezi, TRA ilipanga kukusanya Sh. Trilioni 2.95 na kwamba kiasi hicho ni ongezeko la asilimia 9.2 la makusanyo ya kipindi kama hicho kwa Desemba 2022 ambayo yalikuwa Sh. trilioni 2.97.

Sababu kubwa za kuweka rekodi hiyo ya makusanyo, kwa mujibu wa Kamishna Mkuu Kidata, yalitokana na juhudi za mamlaka katika kutekeleza kwa vitendo maelekezo na miongozo mbalimbali iliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan na viongozi wengine wa serikali.

Mbali na maelekezo hayo, sababu nyingine ya kupaa kwa makusanyo hayo ni utekelezaji wa mpango mkakati wa sita wa TRA ambao pamoja na mambo mengine, umeboresha muundo wa mamlaka ikiwamo uanzishwaji wa divisheni mpya za walipakodi wa kati na wadogo ili kutoa huduma bora na stahiki kwa walipakodi kwa kuzingatia mahitaji yao.

Makusanyo hayo yanaonyesha kuwa mamlaka hiyo imetekeleza kwa mafanikio malengo iliyojiwekea katika kukusanya mapato ya serikali kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo. Pia maboresho yaliyofanyika ndani ya mamlaka, hasa ya kimuundo, yamekuwa chachu katika kufikia na kuvuka malengo hayo.

Pamoja na mafanikio hayo, jitihada zaidi zinapaswa kufanywa ili kukusanya mapato zaidi kwa ajili ya maendeleo na wakati huo huo kupunguza utegemezi wa misaada ya mikopo kutoka kwa wahisani na vyombo vya fedha vya ndani na vya kimataifa.

Yako maeneo mengi ambayo kama TRA itathubutu kuyasimamia ipasavyo, kuna uwezekano wa kuleta matokeo chanya zaidi yanayoonekana sasa. Mfano ni katika eneo la milki ambalo kuna nyumba nyingi za kupangisha lakini mapato yake hayana uhalisia wa kile kinachokusanywa.

Katika Mkoa wa Dar es Salaam, mathalan, kuna nyumba nyingi ambazo zimepangishwa kibiashara lakini jambo la kujiuliza ni je, kiasi kinachokusanywa na TRA kinashabihiana na idadi ya nyumba za kupangisha? Mtu mmoja anaweza kuwa na nyumba za kupangisha (apartment) na anatoza Dola za Kimarekani 2,000 kila moja lakini tujiulize analipa kiasi gani cha kodi?


Ni wazi kwamba eneo hilo linawagusa vigogo wengi wakiwamo maofisa waandamizi wa TRA wenyewe lakini ni nani wa kumfunga paka kengele? Ni vyema eneo hilo likaangaliwa kwa jicho la kipekee kama kweli TRA na serikali kwa ujumla ina dhamira ya kweli katika ukusanyaji mapato.

Jambo lingine ambalo linaweza kuleta ufanisi zaidi katika ukusanyaji mapato ni kujenga mazingira rafiki baina ya TRA na wafanyabiashara. Hili ni eneo ambalo limekuwa likilalamikiwa kwa muda mrefu kiasi cha kuonyesha kwamba uhusiano wa pande hizo ni kama paka na panya.

Kumekuwa na madai kama vile matumizi ya nguvu zikiwamo silaha katika kuwafuata walipakodi na baadhi ya maofisa wa TRA wakafuata walipakodi na kuwabambikia kodi huku wakiwataka kuwalipa kiasi fulani ili wawasamehe! Sasa ni wakati mwafaka kwa TRA kujenga urafiki chanya na walipakodi ili kuhakikisha wanalipa kodi kwa kufuata misingi na taratibu zinazotakiwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

# Ukwapuzi huu wa bodaboda ni tishio

Na Tuntule Swebe

**WIZI** unaofanywa na vibaka au wezi wanaotumia pikipiki ni kero nyingine ambayo inawaacha watu na majonzi kila siku. Ni baada ya kuporwa simu, pochi, mifuko na vitu vingine muhimu vyenye thamani.

Wanaolengwa na wizi huo ni pamoja na wafanyabiashara, wanaotembea pembeni ya barabara na kinamama, hawa wanaoadhibiwa na vijana vibaka ambao huonekana kama madereva wa bodaboda.

Watu huibiwa mijini na hata mitaani na wezi hao wanaoendesha pikipiki kwa kasi ambao wanapomwona mwenye simu anachati huku anatembea wanakwapua simu yake kwa kumsogelea na kukimbia.

Mambo hayaishi hapo hata wale wanaoongea na simu huku wakitembea au kama wamesimama pembeni huporwa na madereva hao wanaojichanganya na wengine muda mfupi baada ya kuiba.

Wengine ni wajanja huiba muda ambao hakuna magari wala pikipiki barabarani na hilo hulifanya kwa ujasiri.

Huiba hata mchana kweupe na jioni giza linapoingia, usiku, alfajiri pamoja na wakati wote vichochoroni, tena pamoja na simu huiba pochi au mabegi ya kinamama pamoja mizigo mingine inayobebeka kwa urahisi.

Wizi unafanyika kwenye njia kuu au barabara kuu ambako wahusika licha ya kuweka maisha yao mashakani hawababaiki. Wanahatarisha maisha yao kwani watu wanaweza kuwashambulia na kuwaumiza na kuuawa wakati wakitoroka.

Mathalani, kuna madai kuwa lipo kundi la wezi ambalo limeundwa na watu fulani ili kujinufaisha na uporaji huo wakiwatumia madereva wa pikipiki. Kundi hilo ambalo baadhi ya vijana huliita 'vishandu' linaripotiwa kufanya uhalifu maeneo mengi hasa Dar es Salaam na inadaiwa kuwa wanaongezeka kwa sababu ya ukosefu wa ajira.

Kwa upande mwingine sikubaliani nao kwa sababu mara kwa mara vijana wanapewa suluhisho la kumudu maisha yao ikiwa ni pamoja na kuelekezwa kufanyakazi.

Wanaweza kujipatia la kufanya kwa kutumia mtaji mdogo na siyo kiasi kikubwa cha pesa mfano wanaweza kuuza mahindi ya kuchoma, mishikaki, vyakula vya aina mbalimbali kuanzia biriyani, uji, vyakula vya asili, chai, juisi na matunda sehemu mbalimbali hasa sokoni na kwenye mikusanyiko.

Wanaweza kushona viatu, mikoba, kukusanya plastiki mitaani badala ya kuyaweka maisha yao hatarini na kupelekea jamii au familia zao kuishi wakiwa na wasiwasi kuhusu maisha yao.

Ni vyema familia, wazazi na walezi kuwa makini na watoto wao kila wakati wasiwaache kuwa na utitiri wa vitu mfano simu janja nyingi, kuuza vitu vilivyotumika kuanzia saa, simu, pochi na waleti bila kuwabana na kujua wanazipata wapi na kama ni za wizi kuchukua hatua.

Ikumbukwe wizi unarudisha nyuma mipango na maendeleo ya watu wengi kuanzia wanaoibiwa hata wezi pia hasa wanapokamatwa au kupigwa kwa kuhisiwa wizi na mwisho kuuawa.

Inasikitisha kwani wizi huu unahusisha hata watoto wadogo au chipukizi wanaoiba simu au mali nyingine kwa kuwapora watu barabarani.

Ni hatari vijana hawa kuingia kwenye kundi la wahalifu katika umri mdogo, tujiulize ni kizazi gani kinaandaliwa? Mbona jamii na familia zinaachia watoto kuharibika kwa kuiga na kufanya maovu?

Mmomonyoko huu wa maadili unazidi kuumiza jamii ambayo licha ya watu kuwa na miili na akili timamu wanaamua kujiingiza kwenye wizi ili kupata riziki.

Watanzania wakumbuke kuwa uhalifu unaharibu sifa ya taifa na kujenga hofu kwa raia na hata wageni wakiwamo watalii.

Ikumbukwe pia kuwa kuna baadhi ya miji na majiji Afrika yanasifika kwa uhalifu hivyo ni lazima vyombo vya ulinzi na usalama wa raia viwe makini, vichunguze, kufuatilia na kukomesha mambo hayo yanaoongeza hofu kwa raia.

Ni vyema sheria, kanuni na taratibu zisimamiwe ili kukabili uhalifu, mathalani inawezekana bodaboda hizo zina namba bandia ambazo hazijasajiliwa, hilo polisi na Mamlaka za Usimamizi wa Usafiri Ardhini (LATRA) na TRA walichunguze.

Kwenye maeneo mitaani wenyeviti wa serikali za mitaa wakishirikiana na wanajamii wawafichue wezi lakini wahamasishe ulinzi shirikishi ili kukomesha kama si kupunguza matukio ya wizi na kuhatarisha maisha ya watoto hao na hata wanajamii.

Ni wakati wa kuendeleza amani na kujenga jamii yenye uaminifu ili watu wasiishi kwa hofu kutokana na wahalifu kutamalaki.

## HABARI KITAIFA

# W'biashara walalamika mitaro kutosafishwa

**Na Thomas Wandiba,** SAUT

BAADHI ya wafanyabiashara katika Mtaa wa Lumumba, jijini Mwanza wamelalamikia tatizo la mitaro ya barabara kujaa taka na kuziba wakati mvua inaponyesha na kuingia katika maeneo yao ya biashara.

Walitoa kilio chao wakati wakizungumza na Nipashe adha wanayoipata mvua iliponyesha kwa muda wa robo saa na kusababisha maji kutuama barabarani na maeneo ya biashara zao.

Mmoja wa wafanyabiashara, Abdalah Madege alisema chanzo cha maji kutuama ni taka zinazotupwa katika mitaro ya barabara zikiwamo chupa na kushindwa kuruhusu maji kupita.

"Maji yanaingia hadi ndani ya maduka na kusababisha kulowanisha bidhaa zetu na kukosa kabisa soko kwani huwa zinaharibika na kutusababishia hasara tumelalamika sana juu ya suala hili, lakini bado halijapatiwa ufumbuzi," alisema Madege.

Wilfred Minani, mfanyabiashara mwingine wa eneo hilo, aliiomba serikali kudhibiti uchafuzi huo kwa kuweka utaratibu wa kusafisha mitaro hiyo kwa kuwa wanalipia fedha za usafi, lakini hawaoni utekelezaji wake.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Mkoa wa Mwanza, Patrick Masagati, amekiri kuwapo kwa adha hiyo na kuwaomba wamiliki wa nyumba za biashara kuzifanyia marekebisho ili ziwe imara.

"Tayari tumewasilisha tatizo hili la mitaro serikalini ili ifanyie marekebisho ya kudumu katika miundombinu inayozunguka maeneo ya wafanyabiashara na kuondoa hasara za mara kwa mara zinazowakabili wafanyabiashara wote," alisema Masagati.

Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla akizungumza katika kikao cha bodi ya barabara mkoani hapa, aliwaagiza wakuu wa wilaya, wakurugenzi pamoja na wenyeviti wa halmashauri kuweka utaratibu wa muda mrefu wa kudhibiti uchafuzi katika mitaro ikiwa ni pamoja na kuweka utaratibu wa kuizubua kila mara kwa kushirikiana na wananchi.

Alisema kazi hiyo haitakiwi kutelekezwa kwa TARURA na TANROADs kwa sababu wana majukumu mengine ya kuhakikisha wanapanua na kuongeza miundombinu na kwamba sio vyema kutumia muda mrefu katika kukabiliana na kuziba kwa mitaro.

**Wilfred Minani, mfanyabiashara mwingine wa eneo hilo, aliiomba serikali kudhibiti uchafuzi huo kwa kuweka utaratibu wa kusafisha mitaro hiyo kwa kuwa wanalipia fedha za usafi, lakini hawaoni utekelezaji wake.**



Meneja wa Benki ya NBC tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Anne Mwaisaka (kushoto), akiwapongeza baadhi ya walimu wa somo la Hisabati katika shule za sekondari zilizopo Jimbo la Ubungo, Dar es Salaam ambao walifaulisha wanafunzi kwa Daraja A katika Mtihani wa Taifa wa kidato cha nne. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chalamila aingilia kati mgogoro wa umiliki hoteli Golden Tulip

**Na Kulwa Mzee**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila ameelekeza familia ya Ladwa kukaa pamoja kumaliza mgogoro wa umiliki wa kampuni ya Indian Ocean Hotels Limited, inayomiliki Hoteli ya Golden Tulip ya Masaki Dar es Salaam kwa haraka badala ya kuvutana polisi na mahakamani.

RC Chalamila alikaa na familia hiyo pamoja na mawakili wao jana ofisini kwake baada ya Jeshi la Polisi kushindwa kusimamia utekelezaji wa hukumu ya mahakama mwishoni mwa wiki iliyopita.

Akizungumza na waandishi wa habari mmoja wa wakurugenzi na mmiliki wa Indian Ocean Hotels Ltd, Dhirajilal Walji Ladwa, alisema RC Chalamila aliwaelekeza kufuata sheria.

"Ametushauri wote familia ya Ladwa tukae kwa pamoja tumalize mgogoro, kama unahitajika msaada wa wana siasa tutapata, mgogoro wa miaka mitano ufike mwisho.

"Wote familia tumekubali, tunakubali pia Jitesh Ladwa ni mwanahisa, tukae tumalize mgogoro tuendelee na biashara.

"Nazungumza kwa niaba ya familia, tunaomba Rais Samia Suluhu Hassan aingilie kidogo tumalize mgogoro haraka, hii shida iishe," alisema Ladwa.

Wakili Patrick Kahesh akizungumzia majadiliano yaliyofanyika, alisema RC Chalamila anakubaliana na uamuzi wa Mahakama, anashauri mgogoro umalizike kwa familia kukaa pamoja, walimalize suala hilo kwa maslahi ya uchumi wa nchi, biashara ziendelee.

RC Chalamila alibeba jukumu hilo baada ya Jeshi la Polisi kushindwa kusimamia utekelezaji wa hukumu ya mahakama.

Hukumu hiyo ilitolewa mbele ya Jaji John Deo Nangela Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara, Novemba 17, 2023.

Uamuzi huo wa Jeshi la Polisi kumtwisha RC Chalamila mgogoro huo uliotangazwa Ijumaa na Mkuu wa Opereshemi Kinondoni, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Noni.

Uamuzi huo ulifikiwa baada mvutano ulioibuka hotelini hapo baina ya pande mbili za wamiliki wa hoteli hiyo zinazovutana kuhusu umiliki wa hoteli hiyo maarufu nchini.

Pande hizo zinazovutana katika umiliki wa kampuni hiyo na hoteli hiyo ni wa mfanyabiashara Jitesh Jayantilal Ladwa, aliyeshindwa kesi ya kupora na kujimilikisha hisa zote za wamiliki wenzake.

Wamiliki wenzake Jitesh walioshinda kesi hiyo ni Dhirajilal Walji Ladwa na Chandulal Walji Ladwa pamoja na mdogo wake Jitesh, Nilesh Jayantilal Ladwa.

Kabla ya Jeshi la Polisi mkoa wa Kipolisi Kinondoni kuuepeleka mgogoro huo kwa RC Chalamila, upande mmoja wa wamiliki walioshinda kesi ya umiliki ya uporwaji wa hisa za umiliki wa hoteli hiyo ulifika hotelini hapo Ijumaa asubuhi kwa ajili ya kuendelea na shughuli zao.

Wamiliki walioshinda walikutana na upinzani kutoka kwa upande ulioshindwa wa Jitesh baada ya walinzi wake aliowaweka hotelini hapo pamoja na watu wengine waliowaita kutoka mitaani kuwafukuza mpaka nje ya geti la hoteli hiyo, upande ulioshinda.

Kutokana na vurugu hizo maofisa wa Jeshi la Polisi Kinondoni waliingilia kati na kuwachukua wawakilishi wa pande zote wakiwamo mawakili wa pande zote na kwenda kufanya mazungumzo Polisi Oysterbay.

Baada ya majadiliano hayo ndipo askari polisi waliporudi hotelini hapo na ACP Noni kutoa maelekezo ya kuhamishia mgogoro huo kwa RC Chalamila.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)

ewura

**KUMB: PPR/2024 - 01/01**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 3 JANUARI 2024

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini zitakazotumika kuanzia Jumatano, tarehe 3 Januari 2024 saa 6:01 usiku. Kwa mwezi Januari 2024, bei za rejareja na za jumla katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ni kama zinavyoonekana katika Jedwali Na. 1 na 2:

**JEDWALI 1: BEI KIKOMO ZA REJAREJA (SHILINGI/LITA)**

| Mkoa | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 3,084 | 3,078 | 3,510 |
| Tanga | 3,064 | 3,219 | 3,556 |
| Mtwara | 3,201 | 3,456 | 3,582 |

**JEDWALI 2: BEI KIKOMO ZA JUMLA (SHILINGI/LITA)**

| Bandari | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 2,950.81 | 2,887.31 | 3,096.85 |
| Tanga | 2,921.21 | 3,042.45 | - |
| Mtwara | 3,044.20 | 3,148.16 | - |

Kupungua kwa bei za mafuta kwa mwezi Januari 2024 ni kwa sababu ya kushuka kwa bei za mafuta (FOB) katika soko la dunia kwa wastani wa asilimia 6.03 kwa petroli na asilimia 7.13 kwa dizeli. Pia kupungua kwa bei za mafuta kumetokana na kushuka kwa gharama za uagizaji wa mafuta kwa wastani wa asilimia 3.72 kwa petroli na asilimia 17.52 kwa dizeli kwa Bandari ya Dar es Salaam na kwa wastani wa asilimia 22.71 kwa petroli na asilimia 22.12 kwa dizeli kwa Bandari ya Mtwara. Bei za mafuta za rejareja kwa kila mji, wilaya na mkoa ni kama zinavyooneshwa katika Jedwali Na.3.

Wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa rejareja wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei zinazooneshwa katika Jedwali Na. 3. Aidha, wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei zinazooneshwa katika Jedwali Na. 2. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yoyote atakayekiuka AGIZO hili.

EWURA inapenda kuwakumbusha wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla na rejareja pamoja na jamii kuzingatia yafuatayo: -

a) bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli kwa eneo husika zinapatikana kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba *152*00# na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

b) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, kifungu namba 166, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta.

c) Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani isipokuwa bei hizo zisizidi bei kikomo (Price cap) au kuwa chini ya bei iliyoruhusiwa (Floor Price) kama zilivyokokotolewa kwa mujibu wa Kanuni za EWURA za Kupanga Bei za Mafuta za Mwaka 2022 zilizotangazwa tarehe 28 Januari 2022 kupitia Gazeti la Serikali Na. 57 na marekebisho ya Kanuni tajwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 761A la tarehe 30 Oktoba 2023.

d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana yakionesha bei za mafuta, punguzo, vivutio vya kibiashara vinavyotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.

e) Wauzaji wa bidhaa za mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa stakabadhi za mauzo kutoka kwenye Electronic Fiscal Pump Printers (EFPP) na wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora unaotakiwa. Stakabadhi hizo pia zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya bidhaa za mafuta ya petroli.

**JEDWALI 3: BEI KIKOMO ZA REJAREJA KWA SHILINGI/LITA**

| Mji/Wilaya/Mkoa | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|
| **Dar es Salaam** | **3,084** | **3,078** | **3,510** |
| **Arusha** | **3,120** | **3,275** | **3,594** |
| Arumeru (Usa River) | 3,120 | 3,275 | 3,594 |
| Karatu | 3,139 | 3,293 | 3,612 |
| Longido | 3,131 | 3,286 | 3,605 |
| Monduli | 3,126 | 3,281 | 3,599 |
| Monduli - Makuyuni | 3,130 | 3,285 | 3,604 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 3,205 | 3,360 | 3,685 |
| **Dodoma** | **3,143** | **3,137** | **3,568** |
| Bahi | 3,150 | 3,144 | 3,576 |
| Chamwino | 3,138 | 3,132 | 3,564 |
| Chemba | 3,169 | 3,163 | 3,595 |
| Kondoa | 3,176 | 3,170 | 3,601 |
| Kongwa | 3,140 | 3,134 | 3,566 |
| Mpwapwa | 3,144 | 3,138 | 3,570 |
| Mpwapwa (Chipogoro) | 3,156 | 3,150 | 3,582 |
| Mtera (Makatopora) | 3,162 | 3,156 | 3,587 |
| Mvumi | 3,149 | 3,143 | 3,575 |
| **Geita** | **3,250** | **3,243** | **3,675** |
| Bukombe | 3,238 | 3,232 | 3,664 |
| Chato | 3,271 | 3,265 | 3,696 |
| Mbogwe | 3,288 | 3,282 | 3,713 |
| Nyang'hwale | 3,265 | 3,259 | 3,690 |
| **Iringa** | **3,148** | **3,142** | **3,574** |
| Ismani | 3,153 | 3,147 | 3,579 |
| Kilolo | 3,153 | 3,147 | 3,578 |
| Mufindi (Igowelo) | 3,167 | 3,161 | 3,592 |
| Mufindi (Mafinga) | 3,158 | 3,152 | 3,584 |
| **Bukoba** | **3,300** | **3,294** | **3,725** |
| Biharamulo | 3,274 | 3,268 | 3,699 |
| Karagwe (Kayanga) | 3,316 | 3,310 | 3,742 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 3,322 | 3,316 | 3,747 |
| Misenyi | 3,308 | 3,302 | 3,734 |
| Muleba | 3,300 | 3,294 | 3,725 |
| Ngara | 3,287 | 3,281 | 3,713 |
| **Mpanda** | **3,242** | **3,236** | **3,667** |
| Mlele (Inyonga) | 3,224 | 3,218 | 3,649 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 3,261 | 3,255 | 3,687 |
| Tanganyika (Ikola) | 3,260 | 3,254 | 3,685 |
| **Kigoma** | **3,246** | **3,240** | **3,672** |
| Buhigwe | 3,245 | 3,239 | 3,671 |
| Ilagala Village (Uvinza) | 3,247 | 3,241 | 3,673 |
| Kakonko | 3,247 | 3,241 | 3,673 |
| Kasulu | 3,256 | 3,250 | 3,681 |
| Kibondo | 3,253 | 3,247 | 3,679 |
| Muyobozi Village (Uvinza) | 3,245 | 3,239 | 3,671 |
| Uvinza (Lugufu) | 3,237 | 3,231 | 3,662 |
| **Moshi** | **3,110** | **3,265** | **3,583** |
| Hai (Bomang'ombe) | 3,113 | 3,268 | 3,587 |
| Mwanga | 3,103 | 3,258 | 3,577 |
| Rombo (Mkuu) | 3,127 | 3,282 | 3,604 |
| Same | 3,096 | 3,251 | 3,570 |
| Siha (Sanya Juu) | 3,116 | 3,271 | 3,590 |
| **Lindi** | **3,214** | **3,469** | **3,569** |
| Kilwa Masoko | 3,238 | 3,493 | 3,544 |
| Lindi-Mtama | 3,219 | 3,474 | 3,587 |
| Liwale | 3,250 | 3,505 | 3,590 |
| Nachingwea | 3,234 | 3,489 | 3,598 |

# TANGAZO

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ruangwa | 3,240 | 3,496 | 3,599 |
| **Babati** | **3,154** | **3,309** | **3,632** |
| Hanang (Katesh) | 3,165 | 3,320 | 3,643 |
| Kiteto (Kibaya) | 3,170 | 3,325 | 3,643 |
| Mbulu | 3,167 | 3,322 | 3,645 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 3,186 | 3,341 | 3,664 |
| **Musoma** | **3,250** | **3,244** | **3,675** |
| Bunda | 3,241 | 3,235 | 3,667 |
| Bunda (Kisorya) | 3,254 | 3,248 | 3,679 |
| Butiama | 3,247 | 3,241 | 3,673 |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 3,263 | 3,257 | 3,688 |
| Rorya (Ingirijuu) | 3,257 | 3,251 | 3,682 |
| Rorya (Shirati) | 3,265 | 3,259 | 3,690 |
| Serengeti (Mugumu) | 3,258 | 3,252 | 3,684 |
| Tarime | 3,258 | 3,252 | 3,684 |
| Tarime (Nyamongo) | 3,264 | 3,258 | 3,690 |
| **Mbeya** | **3,191** | **3,185** | **3,617** |
| Busokelo (Iwangwa) | 3,203 | 3,197 | 3,629 |
| Chunya | 3,201 | 3,195 | 3,626 |
| Chunya (Lupa Tingatinga) | 3,208 | 3,202 | 3,633 |
| Chunya (Makongolosi) | 3,206 | 3,200 | 3,632 |
| Kyela | 3,207 | 3,201 | 3,633 |
| Mbarali (Rujewa) | 3,175 | 3,169 | 3,601 |
| Rujewa (Kapunga) | 3,185 | 3,179 | 3,611 |
| Rujewa (Madibira) | 3,189 | 3,183 | 3,614 |
| Rungwe (Tukuyu) | 3,200 | 3,194 | 3,626 |
| **Morogoro** | **3,109** | **3,103** | **3,535** |
| Gairo | 3,128 | 3,121 | 3,553 |
| Kilombero (Ifakara) | 3,147 | 3,141 | 3,573 |
| Kilombero (Mlimba) | 3,169 | 3,163 | 3,595 |
| Kilombero (Mngeta) | 3,158 | 3,152 | 3,584 |
| Kilosa | 3,128 | 3,121 | 3,553 |
| Malinyi | 3,168 | 3,162 | 3,593 |
| Mikumi | 3,125 | 3,119 | 3,550 |
| Mvomero (Sanga Sanga) | 3,109 | 3,103 | 3,535 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 3,120 | 3,113 | 3,545 |
| Turian | 3,134 | 3,128 | 3,560 |
| Ulanga (Mahenge) | 3,158 | 3,152 | 3,583 |
| **Mtwara** | **3,201** | **3,456** | **3,582** |
| Masasi | 3,217 | 3,472 | 3,608 |
| Nanyamba | 3,215 | 3,470 | 3,607 |
| Nanyumbu (Mangaka) | 3,237 | 3,492 | 3,631 |
| Newala | 3,222 | 3,477 | 3,614 |
| Tandahimba | 3,215 | 3,470 | 3,607 |
| **Mwanza** | **3,234** | **3,228** | **3,660** |
| Kwimba | 3,252 | 3,246 | 3,678 |
| Magu | 3,242 | 3,236 | 3,668 |
| Misungwi | 3,229 | 3,223 | 3,654 |
| Misungwi (Mbarika) | 3,239 | 3,233 | 3,664 |
| Sengerema | 3,267 | 3,261 | 3,692 |
| Ukerewe | 3,294 | 3,288 | 3,719 |
| **Njombe** | **3,177** | **3,171** | **3,602** |
| Ludewa | 3,214 | 3,208 | 3,640 |
| Makambako | 3,169 | 3,163 | 3,594 |
| Makete | 3,207 | 3,201 | 3,633 |
| Njombe (Kidegembye) | 3,197 | 3,191 | 3,623 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 3,174 | 3,168 | 3,600 |
| **Kibaha** | **3,089** | **3,083** | **3,514** |
| Bagamoyo | 3,095 | 3,089 | 3,521 |
| Bagamoyo (Mbwewe) | 3,107 | 3,101 | 3,532 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Bagamoyo (Miono) | 3,126 | 3,120 | 3,551 |
| Chalinze (Msata) | 3,102 | 3,096 | 3,528 |
| Chalinze Junction | 3,098 | 3,092 | 3,524 |
| Kibiti | 3,104 | 3,098 | 3,530 |
| Kisarawe | 3,091 | 3,085 | 3,517 |
| Mkuranga | 3,094 | 3,088 | 3,519 |
| Rufiji | 3,112 | 3,106 | 3,537 |
| **Sumbawanga** | **3,257** | **3,251** | **3,683** |
| Kabwe | 3,285 | 3,279 | 3,711 |
| Kalambo (Matai) | 3,264 | 3,258 | 3,690 |
| Nkasi (Kirando) | 3,280 | 3,274 | 3,706 |
| Nkasi (Namanyele) | 3,271 | 3,265 | 3,696 |
| Sumbawanga Vijijini (Mtowisa) | 3,257 | 3,251 | 3,683 |
| **Songea** | **3,286** | **3,541** | **3,633** |
| Mbinga | 3,299 | 3,554 | 3,646 |
| Namtumbo | 3,277 | 3,532 | 3,638 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 3,324 | 3,579 | 3,656 |
| Tunduru | 3,251 | 3,507 | 3,613 |
| **Shinyanga** | **3,213** | **3,207** | **3,639** |
| Kahama | 3,217 | 3,211 | 3,643 |
| Kishapu | 3,221 | 3,215 | 3,647 |
| Shinyanga Vijijini (Salawe) | 3,227 | 3,221 | 3,652 |
| Ushetu (Kangeme Village) | 3,235 | 3,229 | 3,661 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 3,229 | 3,223 | 3,655 |
| **Bariadi** | **3,231** | **3,225** | **3,657** |
| Busega (Nyashimo) | 3,243 | 3,237 | 3,669 |
| Itilima (Lagangabilili) | 3,231 | 3,225 | 3,657 |
| Maswa | 3,225 | 3,219 | 3,650 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 3,236 | 3,230 | 3,661 |
| **Singida** | **3,175** | **3,169** | **3,600** |
| Ikungi | 3,170 | 3,164 | 3,596 |
| Iramba | 3,187 | 3,181 | 3,612 |
| Itigi (Mitundu) | 3,175 | 3,169 | 3,601 |
| Manyoni | 3,159 | 3,153 | 3,585 |
| Mkalama (Nduguti) | 3,199 | 3,193 | 3,625 |
| **Songwe (Vwawa)** | **3,200** | **3,194** | **3,626** |
| Ileje | 3,204 | 3,198 | 3,630 |
| Momba (Chitete) | 3,210 | 3,204 | 3,635 |
| Songwe - Mkwajuni | 3,207 | 3,201 | 3,633 |
| Tunduma | 3,205 | 3,199 | 3,630 |
| **Tabora** | **3,192** | **3,186** | **3,618** |
| Igunga | 3,192 | 3,186 | 3,618 |
| Kaliua | 3,205 | 3,199 | 3,631 |
| Mpyagula | 3,224 | 3,218 | 3,650 |
| Nzega | 3,203 | 3,197 | 3,628 |
| Sikonge | 3,201 | 3,195 | 3,627 |
| Ulyankulu | 3,203 | 3,197 | 3,628 |
| Urambo | 3,202 | 3,196 | 3,628 |
| Uyui | 3,199 | 3,193 | 3,624 |
| **Tanga** | **3,064** | **3,219** | **3,556** |
| Bumbuli | 3,094 | 3,249 | 3,567 |
| Handeni | 3,084 | 3,239 | 3,535 |
| Kilindi | 3,099 | 3,254 | 3,570 |
| Korogwe | 3,076 | 3,231 | 3,549 |
| Lushoto | 3,085 | 3,240 | 3,559 |
| Mkinga (Maramba) | 3,071 | 3,226 | 3,570 |
| Muheza | 3,068 | 3,223 | 3,556 |
| Pangani | 3,070 | 3,225 | 3,562 |

**Dkt. James A. Mwainyekule**
**MKURUGENZI MKUU- EWURA**

HABARI KANDA YA ZIWA



# H'shauri yatenga mamilioni kusitiri wanafunzi wa kike

**Na Halima Ikunji,** NZEGA

HALMASHAURI ya Mji wa Nzega mkoani Tabora inatenga Shilingi milioni 10 kila mwaka kwa kununua taulo za kike na kuzigawa kwa wanafunzi kwa ajili ya kuwasitiri wanapokuwa kwenye hedhi.

Hayo yamebainishwa juzi na Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri hiyo, Ajali Marumwengu wakati akizungumza na Nipashe.

Marumwengu alisema mpango huo endelevu umelenga kumfanya mtoto wa kike kusoma kwa bidii bila kikwazo.

Alisema taulo hizo zimekuwa zikinunuliwa kila mwaka kwa kutumia mapato ya ndani ya halmashauri hiyo na kusambazwa katika shule zake zote.

Alisema pamoja na kuwasiri, halmashauri hiyo imetimiza lengo lake la kudhibiti utoro wa watoto hao wanapokuwa kwenye hedhi.

"Taulo hizo zimekuwa zikigawiwa kwa wanafunzi wa shule zote 35 za msingi na 16 za sekondari zilizopo katika halmashauri yetu na mpango huu umechochea watoto wa kike kupenda shule tofauti na miaka mingine kabla ya kubuni mpango huo," alisema Marumwengu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Shomari Mndolwa alisema mpango huo unaenda sambamba na juhudi za uboreshaji wa miundombinu ya elimu katika shule zote.

Kwa mujibu wa Mndolwa, katika mwaka wa fedha 2022/23 na 2023/24 wamepokea Shilingi bilioni 4.8 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vipya vya madarasa ya kisasa, matundu ya vyoo, ofisi za walimu na shule mpya.

"Kwa mara ya kwanza tumejenga shule ya msingi ya ghorofa yenye viwango vya juu kwa gharama ya Shilingi milioni 561 pale uwanja wa ndege wa zamani," alisema Mndolwa.

Alisema shule hiyo yenye vyumba vya madarasa 16, jengo la utawala na matundu 28 ya vyoo vya kisasa yamekamilika kwa asilimia 100 na tayari kupokea wanafunzi mwezi huu.

Alisema shule hiyo itasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi katika Shule mama ya Msingi Maporomoko yenye watoto zaidi ya 2,000 na kwa kuanzia 450 waliopo wamehamishiwa katika shule hiyo mpya.

Alitoa wito kwa wazazi na walezi kuhakikisha watoto wao waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwaka huu, wanaripoti shuleni bila kukosa na walimu kufundisha ipasavyo na kulinda miundombinu ya shule hizo.




Kaimu Meneja wa Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, Everjoy Ngomamiti (wa pili kulia), akikabidhi zawadi za mwaka mpya kwa Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Bugarama wilayani Msalala, Beatha Alistide (kushoto), wakati wafanyakazi wa mgodi huo walipotembelea kituo hicho, jana. Wengine ni wafanyakazi wa Barrick Bulyanhulu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Shirika lasaka pesa kulea watoto waliokatisha masomo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHIRIKA la Agape mkoani hapa limeanzisha mradi wa kilimo cha umwagiliaji kwa lengo la kupata fedha za kuwanunulia chakula na kuwasomesha watoto wa kike waliokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali.

Akizungumza na Nipashe jana shambani kwake, Mkurugenzi wake, John Myola, alisema kuwa ana imani kuwa kilimo ni fursa kubwa ya kuwaingizia kipato na kumudu gharama za malezi kwa watoto hao.

"Kwa sasa hali ya kifedha siyo nzuri na hii inaathiri sana katika kuhudumia watoto hao kwa upande wa chakula, hivyo inabidi kujikita kwenye kilimo ili waendelee kupata msaada katika shirika letu," alisema.

Alisema awali alikuwa akiishi na mabinti 57, baada ya hali ya chakula kutokuwa nzuri, 30 aliwarudisha nyumbani kwao na kusalia na mabinti 27.

"Hali ya chakula siyo nzuri kabisa, tumeamua kujikita kwenye kilimo na tutalima mazao msimu mzima iwe masika au kiangazi sisi ni jembe tu, lakini kwa sasa mvua zinanyesha mazao yapo vizuri," alisema Myola.

Alisema msimu wa kiangazi ukianza, wataanza rasmi mradi wa kilimo cha umwagiliaji kwa mazao ya chakula na biashara ili kukabiliana na ukata wa fedha kutokana na kukosa wafadhili.

Alitaja miradi mingine wanayotarajia kuanzisha na kujiingizia kipato kuwa ni ufugaji wa kuku wa biashara.

"Pia tutaanzisha mradi wa ufugaji wa mbuzi wa maziwa na samaki, kwa sasa tupo kwenye mpango wa kutafuta mitaji na tunaomba wadau kujitokeza kutusaidia tuendeleze ukombozi wa mtoto wa kike kielimu na kutimiza ndoto zao," alisema Myola.

Baadhi ya mabinti hao waliwaomba wadau wajitokeze kuwapatia msaada wa chakula ili kukabiliana na njaa wakati wakiendelea na kilimo.

# Kikundi chamwagiwa sifa kwa miradi

**Na Jenesta Jasson,** MISSENYI

KATIBU Tawala wa Wilaya ya Misenyi mkoani Kagera, Mwanaidi Mang'uro amekipongeza Kikundi cha UMKI cha wakazi wa Kijiji cha Kikukwe Kata ya Kanyigo kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alitoa pongezi juzi katika Maadhimisho ya Maendeleo ya mwaka katika kijiji hicho huku akivitaka vijiji vingine kuiga mfano wa kikundi hicho, ikiwamo kuchangia ujenzi wa zahanati.

Alisema wanakijiji hao wamejitahidi kufanya maendeleo katika maeneo yao kwa kushiriki katika ujenzi wa zahanati ya kata, kuleta walimu wa ziada katika shule nne na kuweka maji katika Shule ya Sekondari Kikukwe.

Aliahidi kushirikiana na wakazi wa kijiji hicho kutekeleza mipango yote ya maendeleo kwa mwaka huu.

Awali akisoma taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Katibu wa UMKI, Magreth Domisian, alisema kwa mwaka jana umoja wao pia ulijenga mabweni ya wasichana, kutoa printa katika shule ya sekondari Kikukwe na kupeleka walimu wa ziada katika shule nne kijijini hapo.

Magreth alisema kijiji hicho kimeanzisha kilimo cha parachichi, vanila, ndizi na darasa la kilimo ili wanakijiji wapate elimu na kulima kwa tija.

Alisema kwa mwaka huu wanatarajia kuongeza vitega uchumi kwa kujenga maktaba, kumbi na maduka kwa ajili ya kutunisha mfuko wa chama hicho.

Mwenyekiti wa Umoja huo, Godfrey Mugini, aliahidi kukifanya kijiji hicho kuwa cha mfano na kuomba serikali kumaliza kero zinazowakabili, ukiwamo ubovu wa miundombinu ya barabara.

Diwani wa Kata ya Kanyigo, aliwapongeza wakazi wa kijiji hicho kwa mfano wa kuigwa na vijiji vingine kwenye kata hiyo na kuahidi kufuatilia utatuzi wa kero zao..

Ukurasa 13



**Wazanzibari wanapojiandaa kusherehekea Mapinduzi, Wizara Ustawi wa Jamii yajinasibu kwa mafanikio**

Ukurasa 1 4



**Vita vyao miamba dunia visivyoelekea kwisha**

siasa

JUMATANO JANUARI 3, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

# Kuelekea uchaguzi Serikali za Mitaa; uko tayari? Jichunguze kabla kutia nia

**NA MWANDISHI WETU**

MWAKA huu ni wa uchaguzi wa serikali za mitaa. Wapo wanaopenda kuwa viongozi ili wawaongoze wenzao na kushirikiana nao kutatua changamoto zinazowakabili ili kufikia maendeleo.

Kama ndivyo, anzeni kujipanga, maana wakati wowote kuanzia sasa kipenga kitapulizwa kwa watiania wa ujumbe wa serikali za mitaa, vijiji au vitongoji, wenyeviti wa mitaa, vitongoji na vijijini pia.

Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Ngazi za Vijiji, Mitaa na Vitongoji (2019) zinataja sifa za mgombea wa uongozi katika ngazi hizi kuwa ni lazima awe mkazi wa kitongoji, kijiji au mtaa. Anaweza kugombea uenyekiti au ujumbe wa halmashauri ya kijiji au ujumbe wa kamati ya mtaa endapo ana sifa hizi.

Mosi ni raia wa Tanzania, ana umri wa zaidi ya miaka 21, anafahamu kuandika na kusoma Kiswahili na Kiingereza. Aidha awe na shughuli halali ya kumwezesha kuishi, lakini awe mkazi mwenye makazi kwenye mtaa, kitongoji au kijiji anachokitumia kugombea uongozi.

Jingine kubwa ni lazima awe mwanachama wa chama cha siasa na amedhaminiwa na chama chake. Kuna sharti jingine kuwa ni lazima awe hajawahi kupatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi.

Afya ni muhimu akitakiwa kuwa mwenye afya timamu ya mwili na akili na kwamba asiwe na ugonjwa wa akili akithibitishwa na daktari anayetambulika na serikali au bodi ya utabibu.

Kipaji hicho ni muhimu cha kuzaliwa nacho, mtiania au mgombea wa kuwaongoza wenzake kama unajijua una kipaji cha uongozi, lakini una sifa za kitaaluma ambazo lazima awe nazo mtiania, ni vyema kujiandaa na kushiriki kinyang'anyiro.



Wananchi wanapomchagua kiongozi wana imani naye. Anayechaguliwa awajibike kuwatumikia. **PICHA: MTANDAO**

Elimu ni hitaji kisheria. Kama kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa zinavyosema ni lazima kujua kusoma na kuandika Kiingereza na Kiswahili, pia nyongeza inaweza kuwa kufahamu kuhesabu, ambacho ni kigezo cha msingi kwa kiongozi yeyote yule.

Litakuwa jambo la ajabu kama kiongozi huyo hajaenda shule na wala hafahamu kusoma wala kuandika hata jina lake wala la wadhifa anaougombea ili awe kiongozi, hivyo elimu ni muhimu wala si utajiri wa kumiliki mali kuanzia ardhi, nyumba, maduka na mifugo.

Kuna baadhi ya watu wanaamini katika utajiri hao huenda wasiwe viongozi bora, ikumbukwe dunia ya sasa ni ya sayansi na teknolojia hivi kujua kusoma na kuandika pekee vinatosha? Kujiongeza zaidi ni muhimu ili kuwa katika nafasi ya kuwa kiongozi mwenye upeo na uelewa zaidi wa mambo ikiwezekana hata kuwazidi wale unaowaongoza kwa kuwa na shahada na stashahada.

Ipo sifa nyingine ni siha au afya ambayo kanuni anajali zaidi afya ya akili. Hii ni ya pili na ya msingi kwa kiongozi kumbuka ukiwa mgonjwa wa mara kwa mara hutaweza kutimiza majukumu yako kikamilifu kwa sababu utakuwa pengine hospitali, dhaifu na usiye na nguvu ya kutekeleza kazi zako ikiwamo kukutana na wapigakura na kuweka mikakati ya kujikwamua na umaskini.

Ukweli na uwazi ni jambo muhimu, kiongozi ni lazima awe mkweli na kinyume chake ni uongo. Muongo anaweza kuletea jamii yake madhara kwasababu atasingizia, kuongopa na hata kutunga mambo ambayo hayana ukweli.

Zama hizi watu wengi wanapenda kuwa viongozi ili kupata utajiri, kuna watendaji wanaouza ardhi ya vijiji, ya wananchi, kufanya udhalimu wa kila hali ili kupata pesa na wengine ni 'machampioni' wa rushwa.

Uaminifu ni sifa nyingine ambayo kiongozi huwafikisha wale unaowaongoza katika kile ambacho wao wana imani thabiti kwamba atawafanikishia katika malengo wanayoyatarajia bila kuwasaliti. Masuala ya wizi na uporaji wa mali za umma, kupenda rushwa na hata wengine kuuza mali za vijiji hasa ardhi, viongozi wa serikali za mitaa myakwepe.

Ni kama vile mtu anakupa pesa umtunzie au kuzifikisha kwa ndugu au jamaa yake, anayo imani kwamba pesa hizo zitakuwa salama na atazipata wakati wowote atakapozitaka kutoka kwako bila ya pingamizi wala maelezo tofauti, tena zikiwa salama.

Awe na upeo mkubwa. Hii ni ile hali ya kuona mbali zaidi. Kiongozi anakuwa na jicho la ziada ili kuwafikisha watu wake katika malengo wanayotarajia. Anatakiwa ajue katika mustakabali wa watu wake nini cha kufanya kwa haraka na matatizo ni yepi na nini cha kufanya ili kupiga hatua.

Kushirikiana bila kuwa na upendeleo, makundi wala ubaguzi. Kiongozi ni lazima awe mwenye ushirikiano na watu wake, hataweza kufanyakazi peke yake. Ni lazima ashirikiane na watu wake na kwa kimombo wanaita 'team work' kwa maana ya kushirikiana kuandaa, kutekeleza na kufanikisha majukumu.

Atachagua miongoni mwa watu wake wenye sifa na kuwapa majukumu ili waweze kushirikiana kikamilifu wafikie lengo wanalolitarajia. Wahenga pia wanasema, 'umoja ni nguvu

INAENDELEA UK. 14

# Maana mwaka mpya kwa uchumi-siasa, kulikoni mipango mingi inakwama?




**Na Mwandishi Wetu**

KILA mwaka, mamilioni ya watu hufanya maazimio ya mwaka mpya, wakitumaini kufanya mabadiliko chanya katika maisha yao.

Mambo yanayojirudia mara nyingi ni pamoja na masuala ya afya, kuimarisha kipato, kujifunza mambo mapya kwa maendeleo binafsi na kitaaluma.

Kufanya maazimio au kuweka malengo, ni kama kujiwekea mwongozo binafsi na kuhakikisha umefanikiwa, inasema BBC.

Unapoweka malengo, unajiwekea ahadi na ndoto zako. Yote ni kuhusu kuwajibika na kuchukua umiliki wa uamuzi na matendo yako.

Ukiwa na malengo, unajiwekea mpango wa kukuhamasisha. Lakini kwa nini inakuwa changamoto kwa wengi kutimiza malengo waliojiwekea wenyewe?

**KWANINI KUSHINDWA**

Sababu ya kushindwa kuyafikia maazimio ya mwaka mpya ni pamoja na kuweka yasiyo ya kweli, inaongeza BBC.

Azimio ni kuhusu kile ambacho ungependa kufanya badala ya kile 'unachopaswa' kufanya.

Watu hujiwekea malengo magumu kupita kiasi ambayo hayafikiki haraka, au huweka rahisi kiasi ambacho huwachosha.

Ni muhimu kukagua maazimio yako ili kuona kama yanaweza kufikiwa au lah mapema iwezekanavyo.

KUKADIRIWA

Je, pengine wakati wa kutimiza malengo hayo ni kidogo? Ni malengo yanayoeleweka, yanaendana, inawezekana kuyagawanya kidogo kidogo, yatafanikiwa ndani ya muda ulioweka?

Kumbuka kwamba ili kuweka azimio, lazima ubadili tabia yako, kwa hivyo hakikisha unayolenga ni ya kuridhisha.

**KUKOSA UWAJIBIKAJI**

Kufanya kazi na kocha, mshauri, au mshirika wa uwajibikaji kunasaidia kuhakikisha unapata nguvu na msukumo unaofaa ili kukuwezesha kuwa na ari zaidi na hata kutimiza ndoto kubwa.

Kwa sababu mafanikio ni jambo la muda, unaweza kuwa na uhakika kwamba ukifuata hatua, utafikia malengo yako.

Ili kutimiza malengo epuka watu wanaokukatisha tamaa unapochagua mwenzi wako wa uwajibikaji, na badala yake fanya kazi na watu wanaokuinua na kukutia moyo, hasa unapojihisi unashindwa.

Ukaguzi wa kila wiki au baada ya wiki mbili unakuruhusu kufuatilia maendeleo yako na kubadilisha visingizio kuwa fursa ya mafanikio.

Kinachopimwa kinafanyika na kile kinachofanyika kinaweza kuboreshwa na kufanywa mazoea kwa usaidizi wa mfumo mzuri wa ufuatiliaji.

> 'Kwa nini' nafsi yako ina uhusiano gani wa kihisia? Visingizio vyote hutoweka wakati madhumuni yana nguvu, na mtu hubadilika kwa kawaida kutoka kwa mtazamo usiobadilika kwenda kwa mawazo yanayotekelezeka.

Vizuizi vingi vinavyoonekana vinatokana na mawazo, makisio, hukumu, kufikiria kupita kiasi, na marejeleo ya hapo awali.

Rekodi ya mafanikio husaidia katika kuhakikisha azimio linakuwa endelevu.

**KUKOSA MIPANGO**

Mipango mizuri inahitajika kila wakati kwa utekelezaji. Ni bora zaidi ikiwa utapanga hatua za utekelezaji wa azimio lako, uyagawanye katika sehemu ndogo ndogo na kuyapanga kwenye kalenda ya utekelezaji.

Malengo ya kila wiki na mipango huleta hisia ya kufanikiwa badala ya kuahirisha. Mfano, "ahh, nina mwaka mzima, ninaweza kuanza tena mwezi ujao nikiwa na muda zaidi." Inaonya BBC

Upangaji pia huhakikisha kuwa marekebisho yote muhimu yamepangwa kabla ya wakati, pamoja na uelewa wa changamoto zinazowezekana kutokea.

Hii inaongeza fursa ya kufanikiwa, hasa linapokuja suala la malengo ya muda mrefu.

**EPUKA KUTOKUJIAMINI**

Usiruhusu makosa yako ya zamani kuamuru maisha yako ya baadaye.Baada ya kujifunza kutokana na kushindwa ni wakati wa kufanya kazi.

Kila ushindi mdogo unapaswa kushangiliwa kwa sababu unakupa motisha kufanya kazi kwa bidii ili upate mafanikio makubwa zaidi.

Kujikosoa au kuwa na mashaka hakusaidii kwa sababu kunalenga umakini na nguvu zako zote kwenye "kwa nini siwezi kufanya hivi?"

Unapoboreka, jizoeshe kujihurumia na kujipenda, na usiruhusu kushindwa au kukatishwa tamaa kidogo kugeuka kuwa kushindwa kwa kudumu.

Kumbuka kwamba maendeleo yanafaa zaidi kuliko ukamilifu, na ikiwa unajiamini, unaweza kufikia mengi kwa kupanga vizuri, utekelezaji, kujifunza, kutafuta msaada na mafunzo yanayofaa.

Haijalishi unahisi uzito kiasi gani, jifundishe kujitia moyo na kuendelea mbele.

**KUKOSA MALENGO**

Watu wengi wanashindwa kufikia malengo kwa sababu hayajulikani.

Unaweza kujua unachotaka, lakini huweza kujua jinsi ya kukipata hadi utakapojua kwa nini unakitaka.

Kwa hivyo, kwa nini unafanya maazimio haya? Ni swali muhimu unalofaa kujiuliza kabla ya kujiwekea malengo.

'Kwa nini' nafsi yako ina uhusiano gani wa kihisia? Visingizio vyote hutoweka wakati madhumuni yana nguvu, na mtu hubadilika kwa kawaida kutoka kwa mtazamo usiobadilika kwenda kwa mawazo yanayotekelezeka.

Ni muhimu kuzingatia, kuchukua jukumu, kujitolea na kuelekeza umakini wote ikiwemo nguvu, mawazo na hatua ili kushikamana na maazimio ya mwaka mpya.

Yasiwe magumu sana au rahisi sana na muhimu zaidi, furahia mchakato wa mabadiliko wakati wa utekelezaji.

Kumbuka, washindi na walioshindwa wana malengo sawa; ni kile mtu anachofanya ili kujaza 'pengo' ndicho kinacholeta tofauti kubwa.

**ANGALIA NYUMA**

Bila shaka kulikuwa na mafanikio, changamoto na makosa uliyoyafanya, uzoefu uliokufurahisha na uliokuza ujuzi wako na mambo ambayo hayakukufurahisha katika mwaka 2023.

Ni mambo ya kawaida ambayo hayapaswi kukukatisha tamaa.

Andika mambo haya mahali ili uyatumie kuweka mkakati wako kuwa wa maana kwa ajili ya mwaka mpya.

Angalia masuala unayoyapa kipaumbele katika mipango yako ya mwaka. Ni mambo gani unayopaswa kuyaangalia unapoandaa mipango ya mwaka ujao?

Angalia yale yaliyokuendeleza na yaliyokurudisha nyuma.

Tofautisha mipango yako ya kikazi na kibinafsi.

Kumbuka malengo yako ya kikazi yatakuwa ni tofauti na yale ya kibinafsi, licha ya kwamba yanategemeana. Vinginevyo huenda usifanikiwe kwa kiasi ambacho ulikitarajia.

Malengo yako ya kikazi yatakuwa ni tofauti na yale ya kibinafsi, licha ya kwamba yanategemeana. Vinginevyo huenda usifanikiwe kwa kiasi ambacho ulikitarajia.

# Wazanzibari wanapojiandaa kusherehekea Mapinduzi, Wizara Ustawi wa Jamii yajinasibu kwa mafanikio

## • Pensheni kwa wote, yafaulu vita dhidi ya ukatili

**Na Sabato Kasika**

SHAMRASHAMRA za maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar, zimeanza, huku viongozi wakielezea mafanikio na mambo makubwa yanayowagusa na kunufaisha Wazanzibari tangu mwaka 1964 hadi leo.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, inapotinga katika studio za Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), kuelezea mafanikio yake, Waziri Riziki Pembe Juma, anasema, mapinduzi yaliyoleta uhuru yamefurahisha na yataendelea kumuenzi mwanachi.

Anasema Mapinduzi ya 1964, yanaendelea kuishi hata leo kwa kugusa jamii akikumbusha kuwa baada ya kumng'oa sultan, serikali ilianzisha makazi maalum ya wazee mwaka 1966, kwa upande wa Unguja yakiwekwa Sebleni, kisha mwaka 1982 yalijengwa mengine eneo la Welezo Pemba.

"Baadaye mwaka 1981 yakajengwa mengine Limbani na hadi Novemba mwaka jana, wazee 67 wanaishi katika makazi hayo maalumu. Sasa wizara inatekeleza mpango wa kuwatengenezea vitambulisho maalumu ili wapate unafuu wa huduma za kijamii," anasema Riziki.

Anasema watapewa huduma kwenye afya, kupokea malipo ya pensheni jamii, usafiri katika vyombo vya umma na kuingia katika viwanja na maeneo ya burudani bila bughudha.

"Vilevile wizara yangu imetengeneza vitambulisho 25,000 na tayari wazee 11,814 wameshakabidhiwa vitambulisho vyao na wengine utaratibu wa kuvigawa unaendelea," anasema.

Anasema sera ya Hifadhi ya Jamii 2014 na Sheria ya Wazee nambari 2 ya mwaka 2020 zinazolenga kuimarisha haki na huduma za kiustawi kwa wazee, kuanzishwa mpango wa pensheni jamii na usimamizi wake ni masuala ya kujivunia.

"Lengo la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kuona jukumu la kuwatunza wazee linaimarishwa kadri hali inavyoruhusu, kwani inataka makazi ya wazee yanaimarishwa na huduma zinakuwa bora zaidi," anasema.

### KUIINUA JAMII

Waziri huyo pia anasema, katika kipindi cha miaka hiyo 60, wizara yake imetekeza programu mbalimbali za kitaifa na kimataifa ili kuinua hali ya kijamii na kiuchumi kwa wanawake, wazee, watoto na jamii yote.

Katika utekelezaji wa majukumu hayo, wizara inashirikiana na washirika wa ndani na nje zikiwamo wizara, idara na taasisi za SMZ, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wadau wa maendeleo, sekta binafsi na asasi za kiraia.

"Wizara ina wajibu wa kusimamia utekelezaji wa dhana ya maendeleo ya jamii, usimamizi na utoaji wa huduma za kiustawi, kuongoza mapambano ya kupiga vita udhalilishaji wa wanawake, watoto na jamii kwa ujumla ili kuimarisha usawa wa kijinsia," anasema.

Riziki anasema, hatua hiyo inasaidia kujenga taifa lenye uchumi imara unaozingatia mchango wa wanawake na wanaume na kwamba ili kutekeleza majukumu hayo, wizara imetayarisha nyenzo zikiwamo sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali na kusimamia utekelezaji wake.

"Usimamizi huo ni kwa ajili ya kuweka mustakabali mzuri kwa wananchi katika ngazi zote kushiriki kikamilifu kuleta maendeleo ya mtu mmoja mmoja, familia, jamii na taifa kwa ujumla," anasema.



Waziri Riziki Pembe Juma, akielezea mafanikio ya wizara yake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

### SERA NA SHERIA

Waziri Riziki anasema katika miaka 60 ya Mapinduzi Zanzibar, wizara imeandaa sera, sheria, kanuni na miongozo na kufanyia kazi nyenzo zinazohusu watoto na inasimamia Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2001 na Sheria ya Mtoto nambari 6 ya mwaka 2011.

Riziki anafafanua kuwa, ili kuweka kutekeleza vizuri Sheria ya Mtoto, mwaka 2017 kanuni ya matunzo na hifadhi ya mtoto, kanuni ya makaazi yaliyokubaliwa na kanuni ya malezi zimeandikwa.

"Wizara sasa ipo katika hatua za kuendelea kuifanyia mapitio Sera na Sheria ya Mtoto, ili ziende sambamba na wakati na mahitaji ya sasa, lakini wizara imeendelea kuwawezesha wanawake wajasiriamali na kuwaunganisha na fursa za kiuchumi ili waweze kujikomboa katika kupambana na umaskini na wamepatiwa usajili wa kupata mikopo kupitia taasisi za kifedha kwa ajili ya kuendeleza," anasema.

Aidha, anasema, wizara imeunda kamati na kuandaa miongozo mbalimbali ya kupinga ukatili na udhalilishaji wa kijinsia na kwamba katika juhudi hizo, iliandaa mpangokazi wa kitaifa wa kupambana na vitendo hivyo wa mwaka 2017 hadi 2022.

Tunaendelea kuandaa mpangokazi mpya kwa mwaka 2023 hadi 2028, tunahamasisha na kutoa elimu kwa jamii kupitia vyombo vya habari, tukishirikiana na taasisi za kidini waratibu wa shehia na masheha kutoa elimu ya kupinga ukatili na udhalilishaji kwa jamii," anasema.

Anasema, wizara pia imeanzisha timu ya wanaume wa mabadiliko (Male Champion) ya kuwahamasisha wanaume wenzao ili washiriki kikamilifu katika harakati zote za kupinga ukatili na udhalilishaji katika jamii.

"Tuendelee kuiomba jamii kwa pamoja tuungane kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto. Kama wizara, tunaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kupunguza vitendo hivyo ndani ya jamii," anasema.

### HATUA ZAIDI

Riziki anasema, kibajeti, wizara inazingatia mpangilio wa programu kuu tatu za Hifadhi ya Jamii, Uratibu na Utawala na Maendeleo ya Jamii na Jinsia, na kwamba wizara inaendelea kusimamia na kutekeleza shughuli zake kwa kufuata Mipango ya Kitaifa ikiwamo Dira ya Maendeleo ya 2050 ya Zanzibar; Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020.

"Lakini kuna Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021-2026, wizara inaendelea kutekeleza ahadi za Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi anazozitoa katika vipindi na nyakati mbalimbali," anasema.

Kimataifa, anasema wizara inasimamia utekelezaji wa Mkataba wa Haki za Watoto, (CRC 1989); Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Watoto (1991); Malengo Endelevu ya Dunia (SDGs 2030), Azimio la Beijing (1995) na Azimio la Paris (2021).

"Wizara pia inasimamia utekelezaji wa Ajenda ya Afrika Tuitakayo (2063) ambayo ina lengo la kuiona Afrika inaondokana na vitendo vyote vya ubaguzi na kuleta usawa na ushirikianao," anasema.

Anasema, hatua hiyo itasaidia kuimarisha haki za wanawake na watoto, kuleta uwiano wa pamoja kwa ustawi wa jamii, huku ajenda ikisisitiza ushirikiano wa Jumuiya za Kikanda wa kuwa na Afrika yenye umoja.

Riziki anaongeza kuwa lipo suala la usimamizi wa ajenda ya Jumuiya ya Nchi za Afrika Kusini mwa Afrika (SADC), na kwamba lengo ni kuimarisha ushirikiano wa nchi wanachama unaohusisha kiuchumi na biashara, kuwa na ulinzi na usalama katika nchi husika.

"Wizara imeimarisha ushirikiano wa kisekta na wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kuwa na utekelezaji mzuri wa majukumu," anasema.

Anaongeza kuwa wizara hiyo imefanya makubaliano na taasisi mbalimbali kwa lengo la kufanya kazi kwa pamoja ikiwamo Chuo cha Ustawi wa Jamii Tengeru Arusha.

### CHANGAMOTO

Mbali ya mafanikio yaliyopatikana katika wizara yake, anasema bado inakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwamo matukio yanayokithiri ndani ya jamii na kusababisha kuongezeka kwa ukatili na udhalilishaji.

"Kuna tatizo la kuendelea kwa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto, ongezeko la utelekezaji wa watoto na uwajibikaji mdogo kwa baadhi ya familia," anasema.

Ucheleweshwaji wa upelelezi wa kesi za ukatili na udhalilishaji nao unatajwa na waziri kama miongoni mwa changamoto, ingawa anafafanua kuwa wanaendelea kuzitatua kadri hali inavyoruhusu.

"Lakini nimshukuru Rais wetu Dk. Hussein Mwinyi kwa kuendelea

kutuletea maendeleo na pia kwa kuwa kinara wetu namba moja katika mapambano ya kuzuia ukatili na udhalilishaji wa kijinsia," anasema.

Katika hitimisho la maelezo yake, Waziri Riziki anawaomba wanaume kuiga mfano wa Rais Mwinyi, kwa ajili ya kuepukana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwenye jamii yao.

JUKWAA LA VIONGOZI

# Vita vyao miamba dunia visivyoelekea kwisha

• Israel yaishambulia Hamas; kilio Ukraine kinambeba Putin



Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskyy



Vladimir Putin wa Urusi. **PICHA: MTANDAO**

**Na Gaudensia Mngumi**

VITA vya Urusi na Ukraine ni jambo lisilojulikana hatima yake. Wakati siku zinavyokwenda aliyevamiwa ameanza kuwa na dalili za "uchovu au kuchoka", na hilo linaweza kusababisha kwa urahisi kuibuka maoni kwamba, alifikiria washirika wa magharibi hasa Marekani wangemsaidia, huenda isiwe hivyo.

Waukraine, kupinga uvamizi wa Urusi kunaendelea kuwa changamoto kubwa kwa nchi yao, ingawa hakuna takwimu rasmi juu ya vifo, majeruhi na hasara lakini vyombo vya habari vya magharibi vinakadiria kuwa mwezi Agosti mwaka jana watu 300,000 walijeruhiwa kwa pande zote mbili, wakati 190,000 walikufa, The Guardian ya Marekani inaripoti.

Walakini, ukweli ni kwamba hakuna dalili za Ukraine kushinda vita hivi kwa urahisi. Matarajio ya mafanikio kuwatoa wanajeshi wa Urusi katika ardhi yao si jambo rahisi kama pengine Waukraine walivyokuwa wanadhani hapo awali.

Hata hivyo, wakati huo huo, kuna mzozo mwingine unaoendelea katika Mashariki ya Kati, baina ya Israel na Hamas huko Gaza, ambao bila shaka washirika wa magharibi hawatakuwa na haja ya kuendelea kutoa ufadhili na silaha kwa Kyiv, hivyo nguvu kubwa inaanza kupungua.

Ndani ya mwaka 2024, swali ni hili ikiwa washirika hao wamepoteza moto wa kusaidia kumaliza vita, inamaanisha ni azimio la pamoja au watu wamechoka wakisema vita viendelee bila njia au mikakati ya wazi ya kuvikomesha. Au wapigane hadi mwisho utakapofika.

Vyombo vya habari vya magharibi kama The Guardian, vinapotafakari hali ya Ukraine vinaonyesha kuwa kuna kukata tamaa zaidi huko Kyiv. Vinasema ukiangalia hali ilivyo si rahisi kuizungumza, vita hivyo vilionekana kuwa vingekwisha mapema siku za kwanza, lakini leo sivyo, matumaini yanapungua.

Aidha, vinachambua kuwa kuna matumaini kwa vile watu wengi nchini Ukraine wanaamini kuwa wanaweza kushinda vita iwapo watapata msaada wa kutosha wa kijeshi kutoka nchi za magharibi, swali linabaki inawezekana?

Licha ya mashambulio kadhaa na hata uasi wa majeshi ya mamluki ya Wagner, bado karibu asilimia 20 ya Ukraine iko chini ya udhibiti wa Urusi. Wachambuzi wengi wanaona nguvu ya majeshi ya Urusi yaliyo mstari wa mbele imekita mizizi kwa njia ambayo hufanya mafanikio kushinda vita kuwa magumu kufikirika.

**SINTOFAHAMU**

Sababu ya kuelekea kukata tamaa huko Kyiv ni hisia kwamba upinzani ulikuwa umedhibitiwa lakini haikuwa kweli. Wakati wachambuzi wanasema kwamba vikosi vya Ukraine vilizoea silaha mpya za kisasa tofauti za zile zilizoundwa na Urusi pia na mafunzo, zipo taarifa kuwa kulikuwa na kutoelewana kati ya Kyiv na Marekani juu ya kukusanya vikosi katika eneo kubwa au kuyasambaza zaidi majeshi ili kuchunguza udhaifu wa askari wa Urusi.

Maofisa wa Marekani mfadhili mkuu wa Ukraine kwenye vita dhidi ya Urusi, wanaamini kwamba wanajeshi wa Ukraine walikuwa kwenye maeneo mengi wakifanya mambo mengi kwa wakati mmoja na kwamba hakuna mafanikio makubwa.

Kuna dalili ndogo kwamba kuna upande utakaopiga hatua kubwa au kushinda. Hivi karibuni Urusi inaelezwa kuwa imejenga ngome imara za ulinzi ambazo zinafanya iwe vigumu kwa Ukraine kusonga mbele. Lakini ngome hizo pia zinawazuia Warusi, kwa sababu wanalazimika hata kushindwa kupitia maeneo makubwa walikotega mabomu.

Hata hivyo, askari wanapigana na kufa kila siku, lakini kuna wakati vita vya kutisha vinapiganwa kwenye miji midogo yenye umuhimu mdogo wa kimkakati, hali inayoonyesha hakuna sehemu salama.

**UHABA ASKARI**

Wakati huo huo, Urusi inaelezwa kujiimarisha ikiongeza matumizi yake ya ndege zisizo na rubani kufuatilia mienendo ya wanajeshi wa Ukraine na ina uwezo bora zaidi wa kukabiliana haraka na mabadiliko yoyote ya kimbinu kutoka kwa adui zao wa Kyiv.

Kwa Rais wa Urusi, Vladimr Putin ni rahisi kutuma idadi isiyo na kikomo ya walioandikishwa jeshini hata kupigana hadi kufa bila kulipa gharama yoyote. Tena Urusi inatumia mpaka mamluki wakiwamo Wagner, kinyume chake mambo yanazidi kuwa ngumu kwa Ukraine kuongeza wanajeshi kuziba pengo la waliokufa, waliojeruhiwa na waliochoka kwenye mapigano ya mstari wa mbele.

Wakati mwingine serikali ikaanzisha sera mpya za kutaka watu kujiandikisha na kujiunga na jeshi lakini hata wanaume kutekwa mitaani na kulazimishwa kujiunga na jeshi hilo.

Mwanzoni mwa Desemba mwaka jana, Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskiy, anakaririwa na vyombo vya habari akisema nchi yake inafikiria kuhamasisha watu 500,000 wajiunge na jeshi.

Ikiripoti DW, Volodymyr Zelenskiy anasema kuwa jeshi la nchi hiyo limependekeza kuhamasisha Waukraine kati ya 450,000 hadi 500,000 kujiunga na jeshi katika kile ambacho kitaonekana kuwa hatua kubwa katika vita vyake dhidi ya Urusi.

Idadi kamili ya wanajeshi wa Ukraine haijulikani, ila inasadikiwa kuwa karibu watu 1,000,000 nchini humo wamepewa mafunzo ya kutumia silaha, wakati Urusi imekuwa ikitanua kwa kasi jeshi lake kwenye vita na Ukraine ikieleza kuwa inapanga kuongeza askari hadi milioni 1.5, inaripoti DW Desemba 12, 2023.

**GAZA IMEHARIBU**

Mambo yalivyo sasa inaelekea kwamba vita vya Gaza vimechomoza na kutawala vichwa vya habari na umakini wa kisiasa pote duniani na zaidi katika nchi za magharibi. Hali hiyo inabadilisha uelekeo na kuleta madhara makubwa kwa Ukraine.

Kwa muda mrefu, hapakuwa na kingine kwenye televisheni za Marekani kama CNN, BBC huko Uingereza na DW Ujerumani mbali na taarifa za Ukraine lakini sasa Ukraine haipo kileleni kwenye ajenda za habari za nchi za magharibi, imefifia, habari zinazochukua uzito ni Gaza Israel dhidi ya Hamas.

**KUNYIMWA FUNGU**

Ukweli kwamba umma wa mataifa ya magharibi hauko tena Ukraine bali mahala pengine, ni wazi na unabadilisha hesabu za kisiasa kwa viongozi wa Marekani na Ulaya. Bila shaka kuitosa Ukraine kulithibitika mwezi uliopita, wakati Bunge la Marekani likikata msaada kwa Kyiv pale maseneta wa Republican walipopiga kura kuzuia Dola bilioni 50 za msaada mpya wa usalama kwa Ukraine, ni kwa mujibu wa BBC.

## KUELEKEA UCHAGUZI SERIKALI ZA MITAA UKO TAYARI, JICHUNGUZE UANZE KUTIA NIA

**INATOKA UK. 11**

na utengano ni udhaifu.' Tena hata buibui wakiunganisha nguvu ya kamba za utando wao inaweza kumnasa simba.'

Msimamo, ni kuwa na ile hali ya kutoyumba au kuyumbishwa bali kiongozi unakuwa katika mstari, kwa maana kwamba hubadilika badiliki kwa uamuzi na matendo au matamshi ambayo ama umeyatoa. Sio mara leo kasema hivi na kesho kuja na maelezo mengine.

Kiongozi ni mfano wa kuigwa kwa matendo yake na tabia yake nzuri. Watu wengi watamuiga kwa kazi nzuri anayowafanyia na jinsi anavyowaheshimu wale anaowaongoza.

Akubali kukosolewa au kushauriwa, kiongozi si malaika kwamba hafanyi makosa, la hasha! Kiongozi ni binadamu na si mkamilifu kwamba akifanya kitu basi ni sahihi asilimia mia moja, hapana. Mkamilifu ni Muumba kwasababu yeye ndiye mjuzi wa kila kitu hakosei. Kwa hiyo, mgombea uingie na fikra kuwa ukikoselewa ukubali, ukiri upungufu lakini kama kuna ushauri mzuri uufuate usiwe na kiburi kana kwamba anajua vyote.

Kiongozi asiwe mwenye majivuno, kujiona bora, kuwa na dharau na asiyewajali watu wake. Ni lazima awasikilize wengine na kujali matatizo yao na kuwapa faraja wakiamini kwamba wanaye kiongozi anayewajali na ni mwenzao.



# HABARI DODOMA

## Kijiji chakosa zahanati tangu Uhuru

**Na Paul Mabeja,** KONDOA

WAKAZI wa Kijiji cha Salare kata ya Pahi wilayani hapa Mkoa wa Dodoma wameondokana na kero ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya katika vijiji vya jirani tangu Tanzania ipate Uhuru.

Ahuweni hiyo inakuja baada ya juzi kuzinduliwa kwa zahanati ikiwa na vifaa tiba vya kisasa msaada kutoka Shirika la Qatar Charity iliyoghalimu kiasi cha Shilingi milioni 100.

Akizindua zahanati hiyo, Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alisema msaada huo umekuja wakati mwafaka kwani wakazi hao wamekuwa wakikabiliwa na kero hiyo kwa muda mrefu.

"Wakazi hawa wamekuwa wakifuata huduma za afya umbali mrefu hali iliyokuwa ikihatarisha afya zao hasa wajawazito ambapo hivi sasa wameondokana na kero hiyo mara baada ya zahanati hii kukamilika na kuanza kutoa huduma, "alisema Dk. Kijaji

Alisema msaada huo kutoka katika shirika hilo ni matokeo ya Rais Samia Suluhu Hassan kujenga mahusiano mema na mataifa mengine hali ambayo imesaidia wadau kama hao kuja kusaidia katika sekta ya afya.

"Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuweka mahusiano mazuri ya kidiplomasia na mataifa mengi na hii imesaidia kupata msaada huu wa zahanati ambayo inakwenda kujibu kero iliyodumu katika kijiji hiki kwa muda mrefu," alisema

Alisema pia shirika hilo limesadia katika ujenzi wa miskiti na misaada mingine ya kijamii.

Abubakari Rajabu, mwakilishi wa Shirika la Qatar Charity, alisema msaada huo umetokana na maombi ya wakazi wa kijiji hicho kupatiwa zahanati kutokana na kukabiliwa na adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya.

"Leo hii tumekabidhi zahanati hii kwa uongozi wa Wilaya ya Kondoa ambayo imejengwa kwa Shilingi milioni 70 na milioni 30 imetumika kununua vifaa vya kisasa ambavyo vitatumika kutoa huduma za matibabu,"alisema

Tabu Maulidi, mkazi wa kijiji hicho alishukuru serikali na wadau hao kwa kuwasaidia kupata zahanati hiyo na kuwaondolea kero yao sugu ya kutembea umbali mrefu kupata huduma za afya.

Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Dk.Khamis Mkanachi alisisitiza kuwepo kwa usimamizi wa zahanati hiyo na vifaa tiba ili wananchi waendele kupata huduma stahiki kama ilivyo azma ya serikali.

# Wauguzi, wakunga 4,166 kusaka leseni ya usajili

## •Kufanya mitihani, msajili aonya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAIMU Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) Happy Masenga amewaonya wauguzi na wakunga 4,166 nchini kujiepusha na vitendo vya udanganyifu wanapofanya mitihani ya usajili wa leseni.

Masenga alitoa onyo hilo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mitihani hiyo inayofanyika katika vituo saba nchini.

Alisema huo utakuwa mtihani wa 21 tangu baraza hilo lilipoanza kusimamia lenyewe ingawa tangu mwaka 1953 walikuwa wakisimamiwa na Wizara ya Afya na lengo ni kupima umahiri wa watahiniwa ili kupata wauguzi na wakunga wenye sifa.

Alisema watahiniwa wanatakiwa kufika kwenye vituo walivyojiandikisha kwa ajili ya kufanya mitihani hiyo ili wapewe maelekezo.

"Idadi ya wanaofanya mtihani mwaka huu ni ndogo ukilinganisha na mwezi Desemba mwaka juzi (2022), ambao walikuwa 4,600, lakini kwa mwaka huu tuna watahiniwa 248 ambao walikosa sifa mwaka jana na tutaendelea kuwaacha wasio na sifa hadi watakapopata sifa stahiki," alisema Masenga.

Kwa mujibu wa Msajili huyo, hadi sasa wakunga wenye leseni nchini wapo 49,994 ambao wanaendelea kuwafuatilia kwenye maadili yao hadi wanaokwenda kufanya mtihani.

Akijibu kuhusu matokeo kutoka haraka ili wauguzi na wakunga wawahi kuomba nafasi zaidi ya 500 zilizotangazwa na nchi ya Saudi Arabia, alisema wanafanya kazi kwa kuzingatia misingi yao, hivyo watahiniwa watapewa matokeo kama inavyopaswa.

Alisema kwa watakaoshindwa mitihani wanaruhusiwa kurudia kadri wawezavyo hadi watakapofaulu ndipo watapewa leseni.



Mwendesha bodaboda akipita upande wa barabara usioruhusiwa kwa mwelekeo wa kwenda katika Barabara ya Nyerere jijini Dodoma jana, jambo linaloweza kuhatarisha usalama wake na watumiaji wengine. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TANESCO yakarabati miundombinu Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Singida limeendelea kuboresha miundombinu ili kukabiliana na tatizo la kukatika umeme kutokana na uchakavu wa miundombinu katika baadhi ya wilaya mkoani hapa.

Meneja wa TANESCO wa Mkoa huo, Mhandisi Mwamvita Ally aliyasema hayo juzi wakati wa ukaguzi wa maboresho hayo yatakayofanyika katika Wilaya ya Ikungi, Manyoni na Itigi inakopita njia ya umeme ya Manyoni.

Mwanvita alisema hatua ya shirika hilo kuanza maboresho hayo ilitokana na maombi kwa wateja wao wanaohudumiwa na njia hiyo kuwa na changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara.

"Baada ya kupokea maombi hayo timu ya wataalamu ya TANESCO mkoa kwa kushirikiana na wenzetu kutoka makao makuu tulipita kwenye njia hii ya umeme na kufanya ukaguzi na kugundua changamoto kadhaa zinazosababisha umeme kukatika," alisema.

Mwanvita alisema kutokana na changamoto hizo, shirika hilo lilijiwekea mkakati wa muda mfupi wa kubadilisha vifaa chakavu kwenye njia hiyo kama vikombe ambapo tangu waanze kazi hiyo wiki mbili zilizopita tayari wamebadilisha vikombe 3,000.

Alisema pia wanabadilisha nguzo zilizooza na wana imani baada ya matengenezo hayo changamoto hiyo itamalizika.

Aidha, alisema kuna changamoto nyingine kubwa ya uharibifu wa miundombinu ambayo inafanywa na wananchi katika shughuli zao za kibinadamu wakati wakisafisha mashamba yao ambayo yapo kwenye njia ya umeme na kusababisha kuchoma nguzo na kusababisha hasara kwa shirika hilo.

Meneja huyo alitoa rai kwa wananchi kuilinda miundombinu ya shirika hilo kwani jukumu hilo ni la kila mtu na si shirika hilo peke yake.

Mbunge wa Manyoni Mashariki, Dk. Pius Chaya alisema changamoto kubwa iliyopo kwenye jimbo hilo ni kukatika umeme na kuwa kituo cha kupozea umeme wanachokitegemea ni cha Singida mjini ambapo umeme ukipozwa huko ndio urudi tena Manyoni na kuwa unatembea takribani kilometa 150.

Dk.Chaya alisema kutokana na hali hiyo iwapo kutatokea changamoto yoyote kwenye njia hiyo basi wilaya ya Manyoni inakosa umeme.

Chaya alisema changamoto hiyo inakwenda kumalizika baada ya kumueleza Rais Samia Suluhu Hassan ambapo ametoa Shilingi bilioni 30 kwa ajili ya kujenga kituo cha kupozea umeme katika wilaya hiyo mwaka huu.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Manyoni, Jumanne Mkhandi aliishukuru Serikali kwa kuhakikisha wananchi wanapata umeme wa uhakika kutokana na maboresho yanayoendelea kufanyika kwenye njia hiyo ya umeme.

Ismail alisema mahitaji ya umeme katika wilaya hiyo na nyingine zote ambazo zipo kwenye njia hiyo ni makubwa kutokana na shughuli nyingi za kiuchumi na viwanda kutegemea nishati hiyo, unapokosekana inakuwa ni changamoto kwao.







Katibu Tawala mkoani Songwe, Happiness Seneda, akiwapa zawadi ya daftari na mikebe pamoja na mabegi wanafunzi wenye uhitaji maaluma na wenye ulemavu wilayani Momba jana. Kulia ni Ofisa Elimu mkoani humo, Michael Lugola. **PICHA: YASINI IBRAHIM**

# Wafanyabiashara wa mazao wakacha masoko Makambako

**Na Elizabbeth John,**
NJOMBE

SERIKALI mkoani hapa imeombwa kuwahamishia wafanyabiashara wadogo wa mazao kwenye soko la Maguvani, Kiumba na Magegele badala ya kuwaacha kwenye maeneo yasiyo rasmi na makazi ya watu ya Halmashauri ya Mji Makambako. Ombi hilo limetolewa na baadhi ya wafanyabiashara wa Maguvani lililopo Kata ya Maguvani siku chache baada ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka kuiagiza halmashauri hiyo kuachana na mpango wake wa kuwahamishia kwenye maeneo yasiyo rasmi na kuwapeleka soko la mazao Kiumba.

Wafanyabiashara hao, walisema kauli ya mkuu wa mkoa, imesababisha wafanyabiashara wengi kuhama Maguvani na kurejea kwenye maeneo yasiyo rasmi na kuathiri biashara zao.

“Kama wanataka miji iwe kama kijiji basi sawa waache hii hali iendelee, lakini kama wanataka miji iendelee kukua basi mkuu wa mkoa tunaomba atengue kauli yake,” Aneth Lwiva.

Mfanyabiashara Jane Kuyava alisema kuwa: “ Lengo la mkurugenzi na madiwani wetu ilikuwa ni kupanua mji na sisi kama wafanyabiashara tumeathirika kwa kiwango kikubwa,” alisema.

Mwenyekiti wa Soko la Maguvani, Given Sanga, alisema baada ya agizo la Mkuu wa Mkoa, wafanyabiashara takribani 300 wamehama soko hilo na kwenda maeneo yasiyo rasmi hasa soko kuu.

Katibu wa Soko la Magegele, Anipe Ngailo, alisema maagizo ya Mtaka kutaka wafanyabiashara waachwe huru imesababisha hata magari kuacha kuingia katika soko hilo kushusha bidhaa.

Desemba 18, mwaka jana Mtaka aliitaka halmashauri hiyo kuwaacha huru wafanyabiashara wadogo wa mazao kufanya biashara kwenye maeneo yao ya awali badala ya kuwahamishia Kiumba wakati akijibu malalamiko yao.

# Kada atamba CCM bora duniani

**Na Elizabeth John,**
LUDEWA

KATIBU wa Siasa na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, Josaya Luoga ametamba kuwa chama hicho ni bora duniani kutokana na kuongoza nchi kwa muda mrefu na viongozi kushinda kihalali kwenye uchaguzi.

Luoga aliyasema hayo wakati akizungumza na viongozi kwenye mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM Kata ya Lubonde wilayani hapa.

Akizungumza katika mkutano huo, aliwataka viongozi kuendelea kushirikiana na kukiimarisha chama hicho ili waendelee kushika dola.

“Chama Cha Mapinduzi ni chama bora namba mbili duniani baada ya Chama cha CPC cha China, na hii ni kwasababu ya mfumo wa uongozi, utaratibu wake wa upatikanaji wa uongozi na namna tunavyoshinda uchaguzi,” alitamba na kuongeza:

“Pia ndicho chama namba moja kinachoendelea kuongoza taifa kwenye mataifa yenye mfumo wa vyama vingi vya siasa kwa hiyo Tanzania ndio nchi pekee ambayo ina chama tawala toka nchi iingie kwenye mfumo wa vyama vingi.”

Awali Diwani wa Kata ya Lubonde, Edgar Mtitu alikiomba CCM kuwa na imani na viongozi wa kata hiyo kwa kuwa wameendelea kushirikiana kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo licha kuwepo kwa vikundi vya watu wachache wanajaribu kukwamisha jitihada zao.

Mtendaji wa Kata ya Lubonde, Anna Mwalongo alisema kutokana na ushirikiano uliopo baina yao na viongozi wa ngazi za juu, ameweza kupata miradi inayoendelea kutekelezwa ya sekta ya afya, elimu, maendeleo ya jamii, kilimo na ufugaji.

# BAVICHA wawapasha wanasiasa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

VYAMA vya siasa mkoani hapa vimetakiwa kutembelea vituo vya kulelea watoto yatima na wale wenye mahitaji maalumu badala ya kuishia kuandaa mikutano na kunadi sera zao kwa lengo la kupata kura.

Wito huo ulitolewa na Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo Chadema (BAVICHA) Mkoa wa Njombe, Okoka Mbwilo walipotembelea kituo cha kulelea watoto yatima cha Renato Grandi cha Kanisa la Katoliki na cha Ilembula.

Mbwilo alisema jamii inapaswa kutenga muda wa kutembelea watoto hao badala ya kuwatelekezea walezi wa vituo hivyo.

“ Baraza hili kwa pamoja leo tunatoa mahitaji mbalimbali ikiwemo mbuzi, pampasi, sukari, matunda, dagaa, viungo na vinywaji, “ alisema Mbwilo.

Mkuu wa Oparesheni na Uchaguzi CHADEMA Jimbo la Makambako ambaye pia ni Mwenyekiti wa BAVICHA Mkoa wa Mwanza, Mwalimu Boniface Nkobe, alisema iko haja kwa wizara husika kutenga bajeti kuviwezesha vituo hivyo na watoto wote wanaoishi mazingira hatarishi nchini.

Baadhi ya vijana wa baraza hilo akiwemo Amina Mwinami, Monica Ngela, walisema lengo la kutembelea vituo hivyo ni kuwafariji watoto hao na kusherehekea nao mwaka mpya.

Msimamizi wa Renato Granda, Sista Catherine Kidasi na mlezi wa Ilembula Initha, Onesmo Mdeha walisema changamoto kubwa kwa sasa ni ndugu wa watoto hao kuwatelekeza kwenye vituo.

“Tunashukuru sana kwa msaada huu, lakini changamoto kubwa hapa ni ndugu wa watoto hawa wamewatelekeza kwenye vituo bila ya msaada wowote,” alisema Mdeha.

**Mkuu wa Oparesheni na Uchaguzi CHADEMA Jimbo la Makambako ambaye pia ni Mwenyekiti wa BAVICHA Mkoa wa Mwanza, Mwalimu Boniface Nkobe, alisema iko haja kwa wizara husika kutenga bajeti kuviwezesha vituo hivyo na watoto wote wanaoishi mazingira hatarishi nchini.**



# Shein awasihi Wazanzibar kuyaenzi Mapinduzi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

RAIS Mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amewasihi wananchi visiwani hapa, kuyaenzi na kuyatunza Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 ili yawe endelevu kwa sababu yalimkomboa mnyonge kutoka katika madhila ya wakoloni.

Dk. Shein alitoa rai hiyo jana wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi katika ujenzi wa Soko la Jumbi Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja, ikiwa ni shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi Zanzibar.

Alisema kabla ya Mapinduzi hayo kufanyika Januari 12 mwaka 1964 wanyonge walikuwa hawana haki ya kupata huduma muhimu za msingi ikiwamo masoko.

"Ni muhimu mjue mlikotoka nyuma, haya lazima tuyaseme, tuhimize na tujue tulikotoka," alisisitiza.

Dk. Shein aliwataka Wanzazibar kuwa kitu kimoja katika kuyaendeleza Mapinduzi hayo ili yazidi kuleta tija kwa faida yao na Taifa.

Awali Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serkali za Mitaa, Idara Maalum na Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Issa Mahafudh, alisema ujenzi wa soko hilo ni utekelezaji wa ahadi alizotoa Rais Dk. Hussein Mwinyi wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu uliofanyika nchini mwaka 2020.

Mahafudh, alisema ujenzi huo ulianza Novemba mwaka jana na unatarajiwa kukamilika Machi mwaka huu na kwamba kutakuwa na miundombinu ya majisafi na majitaka, umeme, huduma za kijamii, jengo la mnada na machinjio ya kuku.

Ujenzi wa soko hilo ambao utagharimu kiasi cha Shilingi bilioni 24 hadi kukamilika unatekelezwa na Chuo cha Mafunzo cha Jeshi la Magereza Zanzibar.

## Upenja wapelekewa umeme

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Muhamed Said, amesema mradi wa umeme vijijini ni kichocheo cha ukuaji uchumi nchini.

Said aliyasema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa mradi wa umeme katika Kijiji cha Upenja Chokwe Wilaya ya Kaskazini Unguja, ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema wakazi wa kijiji hicho kwa muda mrefu wamekosa umeme na kukwama kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwamo kilimo.

Alisema katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji walilazimika kutumia jenereta na kuwasabishia hasara, hivyo kupatikana kwa mradi huo kutawawezesha kulima kilimo cha mboga na kuuza katika masoko ya utalii.

Aliwataka wananchi kutumia umeme huo kuhifadhi mazao ya baharini na kulinda miundombinu ya umeme ili isihujumiwe.

Kaimu Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), Khamis Ahmada Fakih, alisema utekelezaji wa mradi huo ni kuhakikisha umeme unasambaa katika maeneo ambayo yalikosa nishati hiyo kwa muda mrefu.

Alisema zaidi ya Shilingi milioni 250 zitatumika kwa ajili ya kukamilisha mradi huo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Rashid Hadid Rashid, alisema serikali itaendelea na juhudi za kusambaza umeme kwa vijiji vyingine 42 vilivyobaki katika mkoa huo ili wananchi wote wapate nishati hiyo muhimu.





Vijana wa UVCCM wakiwa katika matembezi ya kuadhimisha Miaka 60 ya Mapinduzi yalioongozwa na kiongozi mkuu Machano Ali Machano, wakinunua mazao ya baharini aina ya chaza katika Soko la Kikungwi Wilaya ya Kusini Unguja jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jenista asifu kasi ya maendeleo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhagama, amesema miaka 60 ya Mapinduzi Zanzibar imepiga hatua kubwa kwa kuwaletea wananchi visiwani hapa maendeleo bila ya ubaguzi.

Akizungumza jana wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi katika shule ya Mwera visiwani hapa, Jenista, alisema kabla ya Mapinduzi hakukuwa na fursa sawa katika upatikanaji wa huduma za jamii ikiwamo elimu.

Alisema kabla ya mapinduzi hayo shule zilikuwa chache na hivyo elimu ilikuwa ikitolewa kwa misingi ya ubaguzi kutegemea na matabaka.

"Jamii kubwa ya Wazanzibari na watoto kutoka familia za kinyonge wengi wao hawakupata fursa ya kupata elimu. Waliobahatika basi walisoma shule zenye hadhi za chini kabisa," alisema.

Jenista alisema hali ya ubaguzi iliendelea mpaka Januari mwaka 1964, ndipo Wazanzibari waliposhikamana na kuamua kuondoa udhalilishaji na madhila waliyokuwa wakifanyiwa na utawala wa kikoloni.

Alisema Wazanzibari walipambana kumwondoa mkoloni kwa kufanya Mapinduzi ambayo Januari 12, mwaka huu, yanatimiza miaka 60 kwa kupiga hatua mbalimbali za maendeleo.

"Sasa sisi sote tumekomboka kwa ndugu zetu waliojitolea, wakiongozwa na Jemedari wa Mapinduzi Hayati Mzee Abeid Amani Karume (Rais wa kwanza wa Zanzibar). Tunapaswa kuijua vizuri historia hii na kutoisahau katika maisha yetu na pia kutorudi nyuma kwani ndio mafanikio ya maendeleo yetu kwa sasa," alisema.

Alisema kabla ya Mapinduzi hayo, Zanzibar ilikuwa na shule moja ya awali iliyokuwa na wanafunzi 60 na shule 62 za msingi zikiwa na wanafunzi 24,334.

Alisema takwimu za elimu zinaonyesha hadi kufikia mwaka jana, idadi ya shule zinazotoa elimu ya awali zimefikia 891 na wanafunzi 102,098 huku shule za msingi zikiwa zimeongezeka na kufikia 649 na wanafunzi 380,638. Kwa upande wa sekondari, Jenista, alisema Zanzibar ilikuwa na shule tano zenye wanafunzi 1,038 kabla ya Mapinduzi na kwa sasa zimefikia 318 na wanafunzi 110,045.

"Ndugu wananchi, idadi ya watu Zanzibar kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita imeongezeka kutoka watu 1,303,569 mwaka 2012 na kufikia watu 1,889,773 mwaka 2022. Hivyo, serikali imeimarisha mikakati yake kupambana na ongezeko la watu na kuhakikisha hakuna Mzanzibar atakayekosa haki yake ya msingi ya kupata elimu popote alipo," alisema.

Akizungumzia kuhusu ujenzi wa jengo la ghorofa la shule hiyo ya Mwera, alisema ni utekelezaji wa mikakati ya Serikali na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa vitendo.

Alisema shule hiyo ni miongoni mwa shule 25 za ghorofa zinazojengwa katika Kisiwa cha Unguja na Pemba katika mwaka huu wa fedha 2023/2024.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa shule hiyo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Dk. Mwanakhamid Adam Ameir, alisema ni mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kuboresha elimu na kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani na kufikia uwiano wa wasiozidi 45 kwa darasa.

Alisema ujenzi huo unalenga kuhakikisha uwepo wa madarasa ya kutosha yatakayopelekea shule zote kuendeshwa asubuhi badala ya kutwa mara mbili yaani asubuhi na mchana kama ilivyo kwa baadhi ya shule.

Alisema ujenzi wa shule hiyo ambao ulianza Mei mwaka jana hadi kukamilika hivi karibuni, utagharimu Sh. 4,500,000,000 zilizotolewa na Serikali.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa Njombe**
**Usimamizi wa mirathi Na. 136/2013**
**HATI YA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(Kanuni ya 7(2) Kanuni za Usimamizi wa Mirathi katika Mahakama za mwanzo)**

**MUSTAPHA NYAGAWA................Marehemu**
**AMANI MUSTAFA NYAGAWA............Msimamizi**

Mnamo tarehe 16 Mwezi 05 Mwaka 2023, Bw. AMANI MUSTAPHA NYAGAWA wamerejeshwa katika usimamizi na kuongezewa muda wa kusimamia mirathi ya Marehemu MUSTAFA NYAGAWA aliyefariki mnamo tarehe 01 Mwezi wa 08 Mwaka 2013, wakiwa wameahidi kusimamia mirathi ambayo ni Nyumba na Mashamba mbalimbali, na mali nyingine kama zilikuwa zinamilikiwa na marehemu kwa uaminifu kama ilivyoelezwa hapa chini, na kuleta orodha ya mali za marehemu kabla au siku ya tarehe 21 mwezi 10 mwaka 2023.

*Mirathi isimamiwe kwa kufuata sharia za mirathi za kiislamu au kimila.

MSIMAMIZI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DEVOTA MATHEW MINJA** anatangaza kupotelewa na kadi za magari zenye namba za usajili **T 358 DXM, T 485 DYN, T 974 DZA, T 501 EAC, T 334 EAK, T 216 DVL, T 741 DUV na T 831 DTU**. Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/ILA/455/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**FAITH KOKUBELWA LUGAZIA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0218-0031 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **RUGAMBWA SEKONDARI** mwaka 1982. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya polisi: PHQ/DAR/KIN/249/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI MADOGO NAMBA 80 YA 2023**
**JESCA JOHN GAMA ...............MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**
**SUZANA JOHN**
**HUMPHREY ALEXANDER UDOBA....MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA HUMPHREY ALEXANDER UDOBA.**

Popote Ulipo Unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya Morogoro tarehe 16/01/2024 mbele ya Mwenyekiti M.KHASIM wewe mwenyewe binafsi au mtume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 19 mwezi December, 2023.

M. KHASIM
MWENYEKITI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAID MOHAMED ALMAZRUI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **NISSAN SAFARI** yenye usajili **NAMBA: T 501 BJV, CHASSIS NAMBA: WRGY 60660067** na **ENGINE NAMBA: TD42008513T.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/DOD/DOD/13080/2023**


**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**Piga Simu 0677020701**

**KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTE KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.**
**TUPIGIE: +255 - 0677020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Somalia yapinga makubaliano ya Ethiopia na Somaliland

**MOGADISHU, Somalia**

BARAZA la Mawaziri la Somalia limeutangaza mkataba uliofikiwa kati ya jimbo lake lenye utawala wa ndani, Somaliland na taifa jirani la Ethiopia kuwa hauna uhalali na haufai. Kikao cha Baraza la Mawaziri la Somalia kilichoongozwa na Waziri Mkuu Hamza Abdi Barre kilifikia uamuzi huo huku waziri mkuu huyo akisema serikali yake itatumia kila njia ya amani iliyonayo kulinda mipaka na mamlaka yake.

Ofisi ya Rais wa Somalia, Hassan Sheikh Mohamud bado haijazungumza chochote kuhusu hatua hiyo. Lakini rais wa zamani wa Somalia, Mohamed Abdullahi Mohamed, maarufu kama Farmajo, ameandika katika mtandao wa kijamii wa X kuwa makubaliano hayo yanasababisha wasiwasi mkubwa kwa Somalia na Afrika kwa ujumla.

Awali msemaji wa serikali ya Somalia anayeshughulikia masuala ya Somaliland, Abdikarim Hussein Guled alisema serikali ya mjini Mogadishu, itajibu hatua hiyo kwa kutoa kauli kali na thabiti. Hussein aliandika katika mtandao wa kijamii wa X kuwa vitendo vya serikali ya Ethiopia vinajumuisha kupuuza kwa wazi kanuni na mifumo ya sheria ya kimataifa, inayowakilisha ukiukaji mkubwa wa mamlaka ya eneo la Somalia.

Pia alisema hiyo inachangia kudhoofisha maendeleo yaliyopatikana kupitia mazungumzo yanayoendelea kati ya Serikali ya Shirikisho ya Somalia na Somaliland ambayo yalikuwa yanakaribia kufikia azimio.

Makubaliano ya Somaliland na Ethiopia yalisainiwa juzi mjini Addis Ababa, kati ya Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed na Rais wa Somaliland, Muse Bihi Abdi, ambaye alisema haya baada ya kuyasaini: "Tuna furaha sana, na tunamshukuru waziri mkuu wa Ethiopia tunaposaini mkataba huu.

Tunawaruhusu watumie kilomita 20 za Bahari yetu na pia watatutambua kama nchi huru. Watakuwa taifa la kwanza kuitambua Somaliland baada ya kusainiwa kwa mkataba huu wa maelewano," alisema.

Ethiopia, nchi ambayo haina eneo linalounganishwa na bahari, wala bandari, inategemea zaidi nchi jirani ya Djibouti katika biashara yake ya baharini.

Aidha, makubaliano hayo yamesainiwa siku chache tu baada ya serikali kuu ya Somalia na Somaliland kukubaliana kuanza tena mazungumzo ya kutatua mizozo yao, kutokana na juhudi za upatanishi zilizofanywa na Djibouti.

Mshauri wa usalama wa taifa wa Ethiopia, Redwan Hussein alisema makubaliano hayo ya kimataifa yanafungua njia kwa Ethiopia kuendesha shughuli zake za baharini kwenye eneo hilo, na kuiwezesha kuifikia kambi ya jeshi iliyokodishwa katika Bahari ya Shamu, njia kuu ya biashara ya kimataifa.

Kwa mujibu wa Redwan, kwa upande wake, Somaliland itapokea sehemu ya mapato ya Shirika la Ndege la Ethiopia. Hata hivyo hakutoa maelezo zaidi kuhusu hilo.

**DW**



Makazi ya watu pamoja na miundombinu ikionekana kuharibiwa vibaya kutokana na tetemeko la ardhi lililoikumba Japan juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Israel kupunguza majeshi yake Gaza

**TEL AVIV, Israel**

JESHI la Israel limethibitisha kuwa litawaondoa wanajeshi wake kutoka Ukanda wa Gaza, hatua ambayo inaweza kufungua njia ya awamu mpya ya mapigano ya viwango vya chini na ya muda mrefu dhidi ya kundi la wapiganaji wa Hamas. Ilibainishwa jana kuwa kuthibitishwa mpango huo wa kupunguza askari, kumefahamika siku ambapo mahakama ya juu ya Israel ilitupilia mbali kipengele muhimu, cha mageuzi ya sheria yanayotetewa na Waziri Mkuu, Benjamin Netanyahu.

Inaelezwa kuwa ingawa mpango huo hauhusiani na vita vinavyoendelea lakini umekuwa chanzo cha migawanyiko mikubwa nchini Israel na ulitishia utayari wa majeshi ya nchi hiyo kabla ya Oktoba 7,

2023 ambako wanamgambo wa Hamas waliishambulia Israel.

**DW**

## Tetemeko la ardhi Japan waliofariki wafikia 48

**TOKYO, Japan**

IDADI ya watu waliofariki katika tetemeko kubwa la ardhi nchini Japan lililosababisha nyumba kubomoka na kupelekea onyo la

Tsunami sasa wamefikia 48. Kulingana na ripoti za vyombo vya habari vya ndani vifo vyote vimetokea katika mkoa wa Ishikawa, kwenye pwani ya kaskazini magharibi ya Japan, ambacho kilikuwa kitovu cha tetemeko hilo la Jumatatu.

Waziri Mkuu wa Japan, Fumio Kishida alisema takribani wanajeshi 1,000 wa nchi hiyo wako katika juhudi za utafutaji na uokoaji wa watu katika maeneo yaliyokumbwa na tetemeko.

Wakati onyo la tsunami likiondolewa, Kishida alisema watajaribu kuanzisha njia za baharini ili kufikia sehemu za mbali za rasi ya kaskazini ya Noto, ambako tetemeko la ardhi lilipiga.

**BBC**

## Kiongozi upinzani Korea Kusini achomwa kisu

**BUSAN, Korea Kusin**

KWA mujibu wa shirika la habari la Yonhap, kiongozi wa upinzani nchini Korea Kusini amechomwa kisu katika mkutano na waandishi wa habari katika mji wa Busan.

Kiongozi huyo anaetambulika kama Lee Jae-myung, ambaye alikosa nafasi ya urais wakati wa uchaguzi mkuu wa 2022, alichomwa kisu upande wa kushoto wa shingo yake majira ya asubuhi jana. Ilielezwa kuwa baada ya tukio hilo mshambuliaji alikamatwa katika eneo la tukio, huku Lee akipelekwa hospitali mara tu aliposhambuliwa. Na kwamba alikuwa katika hali mbaya wakati huo.

Ilibainishwa kuwa alietekeleza shambulio hilo ambaye jina lake halikubainishwa alikuwa ana kati ya miaka 50 au 60, ikielezwa kuwa alikuwa amemkaribia Lee ili kumuomba saini yake, kabla ya kumchoma kisu.

Picha za Video zinazoonyesha shambulio hilo zimesambaa kwenye mitandao ya kijamii zikimuonesha Lee akianguka katikati ya mkusanyiko wa watu, wakati baadhi ya watu wakijaribu kumkamata mshambuliaji. Ilielezwa kuwa picha zilionyesha tukio hilo la kushambuliwa Lee lying akiwa amelala chini huku amefumba macho huku mtu mmoja akiwa amemuwekea kitambaa katika shingo.

Lee ambaye anaongoza chama cha Democratic Party of Korea, anatarajiwakuwania uongozi katika uchaguzi ujao unaotarajia kufanyika mwezi Aprili 2024.

**BBC**

# KARABAKA AFUNGUA SOKO SIMBA KWA WACHEZAJI JKU

Na Adam Fungamwango

BAADA ya kumchukua kiungo mshambuliaji, Saleh Karabaka, aliyefunga bao katika mechi yake ya kwanza tu akicheza dhidi ya timu yake ya zamani JKU juzi kwenye Uwanja wa Amaan Sports Complex, Zanzibar, Klabu ya Simba imeonekana kunogewa na wachezaji wa timu hiyo, kwani jicho lake sasa lipo kwa mchezaji Gamba Idd Matiko.

Taarifa kutoka mjini Zanzibar zinasema katika mechi za Kombe la Mapinduzi ambazo mchezaji huyo amebahatika kucheza, ameonekana kuwavutia mabosi wa Simba pamoja na benchi la ufundi, hivyo wamerejea tena kwa viongozi wa JKU kuangalia uwezekano wa kumsajili pia mchezaji huyo, mwenye uwezo wa kucheza winga zote mbili na mshambuliaji wa kati pia.

"Huku Zanzibar kuna wachezaji wana vipaji sana, siyo Simba tu hata baadhi ya makocha wa klabu mbalimbali wapo huku kuangalia wachezaji wa kuwasajili hasa kipindi hiki ambacho dirisha dogo la usajili lipo wazi, mabosi na benchi la ufundi baada ya kumchukua Karabaka, wameona mali nyingine, wameanza harakati za kutaka kumsajili Gamba na wanaonekana hawatanii kwa sababu wanajua wakimuacha atasajiliwa na timu zingine kwa sababu mchezaji akionekana ana maongezi na timu hiyo basi kila mtu anapiga jicho," kilisema chanzo.

Gamba ambaye amepitia klabu za Mlale JKT, Mbeya City na Mawenzi Market, ni mchezaji wa Timu ya Taifa ya Vijana chini ya miaka 20.

Akizungumza akiwa mjini Zanzibar, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, alisema hawezi kusema lolote kuhusu hilo, lakini klabu yao inaweza kumsajili mchezaji yeyote ambaye inaona anaweza kuwafaa kwenye kipindi hiki na kijacho, huku akimwagia sifa mchezaji wao mpya Karabaka.

"Ni kijana mdogo umri wa miaka 23, tumemsajili kutoka JKU, ni kipaji halisi cha mpira, tulipomtambulisha kuna watu waliguna kwa sababu mchezaji ni mpaka wamfahamu wao, sisi tulimfahamu tangu zamani, ameingia tu na kufunga bao, tena akiwa amefanya mazoezi siku moja tu na timu, umeona kuna wakati alikuwa anatafuta nafasi ili wenzake wampelekee mpira, lakini kwa sababu hawajazoeana ilishindikana.

"Kama itatokea yupo mwingine ambaye tutaona anaweza kuichezea Simba tutamchukua, tunataka wachezaji wenye vipaji ambao ni vijana kwa malengo ya sasa na ya baadaye," alisema Ahmed.

Karabaka alifunga bao la tatu, Simba ikiisulubu JKU mabao 3-1.

Wakati huo huo, Meneja Habari huyo amesema wachezaji wengine wawili wa Simba, Kennedy Juma na Israel Mwenda ambao hawakuambatana na timu kwa sababu mbalimbali, wamewasili Zanzibar na wanaweza kuonekana katika mechi ya leo kama ratiba inavyoonesha dhidi ya Singida Fountain Gate endapo kocha ataona inafaa.

# APR, JKU vita vya walioshindwa leo

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

HUKU akilia kubana kwa ratiba ya michuano ya Kombe la Mapinduzi, Kocha Mkuu wa timu ya APR FC, Thierry Frager, wachezaji wake wanapaswa kujua nini wanatakiwa kufanya uwanjani ili kupata matokeo leo dhidi ya JKU SC.

APR ambayo ilipoteza mchezo wake wa kwanza kwa mabao 3-1 juzi dhidi ya Singida Fountain Gate, leo itashuka tena katika Uwanja wa Amaan Sports Complex kuvaana na JKU ambayo nayo siku hiyo ilipokea kichapo kama hicho kutoka kwa Simba.

Akizungumza na Waandishi wa habari kuelekea mchezo wake wa pili dhidi ya JKU SC, Frager alisema wachezaji wake wamechoka na hawakupata muda wa kupumzika ili kufanyia kazi makosa madogo ambayo ameyaona, lakini kutokana na uzoefu wa nyota wake anaamini watapata alama tatu leo.

Alisema kikosi chake kina wachezaji wazuri na wenye uzoefu, hivyo kubana kwa ratiba na kukosa mapumziko hakutakuwa na athari kubwa sana kwao katika kutimiza malengo yao.

"Tunaenda katika mchezo wetu wa pili, si rahisi sana maana wapinzani wetu wamepoteza michezo miwili mfululizo, hivyo haitakuwa rahisi kuona wanapoteza mchezo wao wa tatu, lazima watahitaji ushindi hivyo lazima na sisi tushinde,"alisema.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa JKU, Khatib Omar, alisema kufanya vibaya katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi kumetokana na kutofanya maandalizi mapema.

Alisema timu yake haikujiandaa kwa mashindano hayo mara baada ya kumaliza michezo ya mzunguko wa kwanza ya Ligi Kuu Zanzibar, na kwamba ni vigumu mchezaji ambaye alishapewa mapumziko kurudi mchezoni hafla. Aidha, alisema licha ya changamoto ya kukosa maandalizi, lakini pia kuna tatizo la ratiba kubana ambayo haiwapi mapumziko, jambo ambalo litakuwa gumu kupata alama tatu katika mchezo huo.

"Mchezo utakuwa mgumu kwa timu zote, kwa sababu sisi hatutaki kufungwa mechi hii ya mwisho katika hatua ya makundi na wenzetu pia wanataka kushinda ili waweze kuwa na uhakika walau wa kusonga mbele," alisema Omar

Timu hizo zitavaana katika Uwanja wa Amaan Sports Complex majira ya saa 10 alasiri na kisha utafuatia mchezo kati ya Simba na Singida Fountana Gate uwanjani hapo saa 2:15 usiku.

**TUTA...**




Mohamed Salah akipiga penalti kwenye mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Newcastle United iliyopigwa usiku wa kuamkia jana katika Uwanja wa Anfield na timu yake ya Liverpool kushinda mabao 4-2. **PICHA: MTANDAO**

# Mbio za urafiki Tanzania, India kufanyika Kitulo

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imesema mbio ndefu za urafiki kati ya Tanzania na India msimu ujao zinatarajiwa kufanyika katika Hifadhi ya Kitulo iliyopo mikoa ya Mbeya na Njombe.

Akizungumza wakati wa kuhitimisha mbio za siku mbili jijini Dar es Salaam juzi, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, alisema wameamua kuzipeleka mbio hizo katika Hifadhi ya Kitulo ili kuhakikisha wakimbiaji wanapata fursa ya kufanya utalii.

Alisisitiza kwamba mbio za mwaka huu zimekuwa na mafanikio makubwa kutokana na kuongozwa na Mkongwe wa Riadha kutoka India, Milind Soman, ambaye aliongozana na familia yake ambapo walikimbia kilometa 120 kutoka Dar es Salaam hadi Bagamoyo kwenda na kurudi.

Dk. Ndumbaro alisema pia maamuzi ya serikali kuzipeleka mbio hizo katika Hifadhi ya Kitulo, yatasaidia kuvutia watalii mbalimbali kuja nchini.

"Tunaratajia mbio ndefu msimu ujao zitafanyikia katika Hifadhi ya Kitulo, kuhakikisha tunavutia watalii mbalimbali.

"Tumepokea wageni kutoka India ambao wamekuja kutembelea sehemu mbalimbali hivyo tutaendelea kushirikiana kati yetu na nchi hiyo.

"Kutokana na ushirikiano huo katika maeneo ya michezo na kuhakikisha mbio hizi zinakuwa na mafanikio makubwa, msimu ujao zitafanyikia Kitulo ambapo kuna bustani ya maua na wanyama rafiki na zitafanyika wiki ya kwanza ya mwezi Julai na zitakuwa endelevu," alisema Dk. Ndumbaro.

Naye Balozi wa India hapa nchini, Binaya Pradhan, aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa kukubali kushirikiana kuandaa mbio hizo.

Alisema mbio hizo zinatarajiwa kuwa endelevu kila mwaka baada ya kutia saini mkataba wa ushirikiano kati ya Tanzania na India.

Alisema msimu ujao wanatarajia mbio hizo zitakuwa na mafanikio makubwa ikiwamo kushirikisha wanariadha wengi kutoka nchi mbalimbali ambao watapata fursa ya kutembelea vivutio vya utalii ikiwamo kupanda Mlima Kilimanjaro.

"Tunaishukuru serikali ya Tanzania kwa kukubali kushirikiana na India kuandaa mbio hizi katika msimu wa kwanza.

"Tunatarajia mbio za msimu ujao zitakuwa na mafanikio makubwa ikiwamo kukusanya wanariadha kutoka nchi mbalimbali kuhakikisha wanakuja kutembelea vivutio ikiwamo Mlima Kilimanjaro," alisema Balozi Pradhan.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE ATAKIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL na Real Madrid zinamtaka mshambuliaji wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu. Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 25, yuko huru kusaini klabu nyingine mwezi huu. **(Le Parisian)**

### PHILLIPS KUTUA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inawania saini ya kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 27, kutoka Manchester City mwezi huu. **(Telegraph)**

### KIMMICH AWINDWA UNITED

KLABU ya Manchester United na Liverpool zinaongoza mbio za kuwania saini ya kiungo wa kati wa Ujerumani, Joshua Kimmich mwenye umri wa miaka 28, mkataba wake na Bayern Munich utamalizika mwishoni mwa msimu huu. **(AS)**

### HEE-CHAN AFIKIRIWA SPURS

LIVERPOOL na Tottenham Hotspur zinafikiria kumnunua mshambuliaji wa Wolves na Korea Kusini mwenye umri wa miaka 27, Hwang Hee-Chan. **(Football Insider)**

### DIER ATAKIWA WEST HAM

KLABU ya West Ham imewasiliana na Tottenham Hotspur kuhusu kumnunua beki wa England, Eric Dier, ambaye yuko nje ya uwanja tangu kuwasili kocha Ange Postecoglou. **(Football Transfers)**

### YORO AFUATILIWA CITY

MANCHESTER City ni miongoni mwa timu zinazomfuatilia mlinzi, Leny Yoro mwenye umri wa miaka 18, huku Lille ikitaka pauni milioni 78. **(Manchester Evening News)**

### ZIYECH KUREJEA CHELSEA

WINGA wa Morocco, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 30, anaweza kurejea Chelsea mwezi huu kwani Galatasaray inapanga kusitisha uhamisho wake wa mkopo wa msimu mzima. **(NTV Spor)**

### LIVERPOOL KWA MARTEN

LIVERPOOL inamfuatilia kiungo wa kati wa Genoa raia wa Denmark, Morten Frendrup mwenye umri wa miaka 22, lakini uhamisho wa Januari huenda usifanikiwe. **(Liverpool Echo)**

### NAVAS ATAJWA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest imeanza mazungumzo na Paris St-Germain kuhusu kumsajili tena kipa wa Costa Rica, Keylor Navas mwenye umri wa miaka 37, ambaye alitumia nusu ya pili ya msimu uliopita kwa mkopo kwenye Uwanja wa City Ground. **(Football Insider)**

### SANTOS ANUKIA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inamtaka mlinzi wa Chelsea mwenye umri wa miaka 19, Mbrazil Andrey Santos, ambaye usajili wake kwa mkopo kule Nottingham Forest unatarajiwa kusitishwa mwezi huu. **(Football 365)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SALAH ANOGESHA MBIO KIATU CHA DHAHABU EPL

●●● Nimetulia, najaribu kufanya kazi yangu na huwa nafanya mazoezi...

**LIVERPOOL, England**

MOHAMED Salah amefikia idadi sawa ya mabao na Erling Haaland katika mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu England, wakati alipofunga mara mbili kwenye ushindi wa 4-2 wa Liverpool dhidi ya Newcastle United, huku akikosa penalti kipindi cha kwanza juzi, Jumatatu.

Mabao mawili ya Salah, ikiwa ni pamoja na penalti kipindi cha pili, yalimfanya mchezaji huyo wa Kimataifa wa Misri kufikisha mabao 14 kwenye ligi msimu huu katika mchezo wake wa mwisho akiwa na Liverpool, ambao walisonga kileleni kwa pointi tatu, kabla ya kutimkia Ivory Coast kwenye michuano ya Mataifa ya Afrika, Afcon.

Lakini baada ya mlinda mlango wa Newcastle, Martin Dubravka, kuokoa penalti yake kipindi cha kwanza, Salah alisema kwamba alibadilisha viatu vyake wakati wa mapumziko ili kuepuka kushindwa kucheza vizuri.

„Ndiyo nilifanya hivyo," alisema Salah akiiambia Sky Sports alipoulizwa kama alikuwa amebadilisha viatu vyake.

"Huwa nakosa penalti ni jambo la kawaida, kwa sababu nacheza na viatu vingi, nikiona hakifai huwa nabadilisha!

„Lakini sipendi kwenda katika kipindi cha pili cha mchezo huu nikifikiria ‚sikufunga bao na hili.' Kwa hiyo niliifanya akili yangu itulie na kuelekeza nguvu kwenye mchezo, inabidi tutulie."

Salah sasa amekosa penalti nne kati ya 10 zilizopita akiwa na Liverpool, lakini alisema hakuwa na nia ya kuacha kupiga wakati mwamuzi, Anthony Taylor alipotoa penalti ya pili baada ya dakika ya 86.

„Nimetulia, najaribu kufanya kazi yangu na huwa nafanya mazoezi," alisema Salah.

"Ya kwanza nilichanganyikiwa kwa sababu kipa alikuwa anasonga na alikuwa anapunga mkono nikawaza, 'sawa twende katikati'. Alifanikiwa kuokoa vizuri sana.

„Ya pili nilifanya nilichofanya kwenye mafunzo na kufanya mambo yangu."

# VARANE ATOSWA MAN UNITED




**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imeamua kutoongeza mwaka mmoja katika mkataba wa Raphael Varane, kwa mujibu wa ESPN.

Inamaanisha kuwa beki huyo anaweza kufanya mazungumzo na klabu nyingine na huenda akaondoka Old Trafford kwa uhamisho wa bure msimu wa majira ya joto.

Varane bado anachukuliwa kuwa sehemu muhimu ya kikosi na kocha Erik ten Hag, lakini United wanasita kuanzisha chaguo la mwaka mmoja ambalo litamfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, kulipwa mshahara wa zaidi ya pauni 300,000 kwa wiki hadi Juni 2025.

Klabu hiyo haijakataa kurefusha muda wa kubakia kwa mchezaji huyo wa zamani wa Kimataifa wa Ufaransa, lakini mazungumzo kuhusu mkataba mpya hayawezi kufanyika.

Mkataba wa sasa wa Varane unatarajiwa kumalizika Juni 2024. Mbinu hiyo ni sawa na ile aliyochukua mlinda mlango wa zamani David De Gea msimu uliopita.

United waliamua kutoanzisha chaguo la mwaka mmoja katika mkataba wa golikipa huyo na aliihama klabu hiyo kwa uhamisho wa bure msimu uliopita.

Varane na De Gea walikuwa miongoni mwa waliolipwa fedha nyingi zaidi United msimu uliopita, pamoja na Casemiro na Jadon Sancho.

Marcus Rashford alijiunga nao alipotia saini mkataba mpya wa muda mrefu Julai na kumfanya alipwe mshahara wa pauni 315,000 kwa wiki.

United inatazamiwa kuongeza muda wa mwaka mmoja kwa Victor Lindelof na Aaron Wan-Bissaka ili kuwaweka wawili hao Old Trafford hadi 2025. Mikataba yao ilitarajiwa kuisha msimu ujao wa joto.

Anthony Martial pia ana mkataba hadi msimu wa majira ya joto, lakini United wameamua kutoanzisha chaguo la kuongeza hadi 2025.

# Partey, Lamptey watemwa Ghana

**ACCRA, Ghana**

GHANA iliwaacha nje Thomas Partey wa Arsenal na Tariq Lamptey wa Brighton kwenye kikosi chao cha wachezaji 27 walioteuliwa kwa ajili ya fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika katika nchi jirani ya Ivory Coast, zitakazoanza baadaye mwezi huu.

Kuachwa kwa Partey kunakuja huku Kocha wa Ghana, Chris Hughton, akisema amepewa muda zaidi wa kupona jeraha la misuli ya paja.

„Pamoja na jeraha lake, bila shaka angekuwa kikosini. Tunajua ubora wa mchezaji alivyo. Huyu ni mchezaji ambaye ana jeraha kubwa," alisema Hughton akiwaambia waandishi wa habari.

„Nimetumia muda mwingi katika kipindi hiki na Thomas na pia kujihusisha na madaktari wa Arsenal.

"Hili ndilo jeraha kubwa zaidi alilopata. Jambo muhimu zaidi kwangu kama kocha mkuu na ni kumpa matibabu na msaada anaohitaji katika kipindi hiki cha muda."

Lamptey alijeruhiwa akiichezea Brighton Novemba, baada ya kocha Roberto de Zerbi kusema kuwa atakuwa nje kwa „kipindi kikubwa".

Ghana wamemjumuisha Andre Ayew kwenye kikosi, jambo ambalo lina maana kwamba atacheza michuano ya Kombe la Mataifa kwa mara ya nane tangu alipocheza kwa mara ya kwanza mwaka 2008. Ameshiriki katika kila mchuano tangu 2013.

Washindi mara nne Ghana watachuana katika Kundi B kwenye Kombe la Mataifa, wakianza na mechi dhidi ya Cape Verde Januari 14 na kisha kukutana na Misri na Msumbiji.






# De Beek atua rasmi Frankfurt

**FRANKFURT, Ujerumani**

KIUNGO wa kati wa Manchester United, Donny van de Beek, amekamilisha uhamisho wa mkopo kwenda Eintracht Frankfurt kwa mujibu wa ESPN.

Kiungo huyo amejiunga na timu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, hadi mwishoni mwa msimu huu.

Frankfurt itailipa United ada ndogo ya mkopo na kugharamia sehemu kubwa ya mshahara wa Van de Beek.

Pia kuna chaguo la kumnunua lililojumuishwa katika makubaliano yaliyowekwa kwa euro milioni 11 pamoja na euro milioni tatu katika nyongeza zinazowezekana.

Van de Beek amevumilia hali ya kufadhaisha kutokana na uhamisho wake wa pauni milioni 40 kutoka Ajax mwaka 2020.

Amecheza mara mbili pekee msimu huu na ameichezea United mechi 12 katika mashindano yote tangu kuanza kwa msimu wa 2022-23.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Uholanzi alitumia kipindi cha pili cha msimu wa 2021-22 kwa mkopo kule Everton, lakini alicheza mechi saba pekee.

Alifika Old Trafford akitoka kuisaidia Ajax kufika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019 chini ya kocha wa sasa wa United, Erik ten Hag.

Alitajwa kwenye orodha ya walioteuliwa kuwa mchezaji bora wa Ballon d'Or mwaka 2019, lakini amecheza mechi sita tu za Ligi Kuu England ndani ya miaka mitatu na nusu akiwa United.

Ana mkataba katika klabu hiyo hadi Juni 2025.

HABARI MICHEZO

# MALKIA WA SIMBA, YANGA VITANI DABI YA KARIAKOO

**Na Saada Akida**

DAKIKA 90, leo zitaamua nani mbabe katika ‚Derby' ya Kariakoo kati ya Simba Queens na Yanga Princess, mchezo wa mzunguko wa tatu wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara.

Simba Queens ambao ni wenyeji wa mchezo huo, itawakaribisha Yanga Princess katika Dimba la Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam majira ya saa 10:00 alasiri.

Kwa msimu huu timu hizo zinakutana mara ya pili, mara ya kwanza ikiwa ni kwenye nusu fainali ya Ngao ya Jamii ambapo Simba Queens alishinda kwa mikwaju ya penalti 5-4 baada ya dakika 90 kukamilika kwa sare ya bao 1-1.

Simba Queens ilisonga mbele na kutwaa Ngao ya Jamii kwa kumfunga Bingwa Mtetezi wa Ligi Kuu, JKT Queens huku Yanga Princes ikiibuka mshindi wa tatu baada ya kuifunga Fountain Gate Princess.

Simba Queens na Yanga Princess tayari zimecheza mechi mbili na kila moja kushinda zote, hivyo leo zinashuka dimbani zikiwa na alama sita mkononi.

Kila timu ipo imara katika safu yake ya ushambuliaji, Simba Queens katika michezo miwili ya ligi hiyo imefunga mabao 10 na kuruhusu mawili, wakati Yanga Princess wakitikisa nyavu mara nane na kuruhusu bao moja.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Msaidizi wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', amesema ni mechi ngumu na ya ushindani mkubwa kwa sababu timu zote mbili zinahitaji pointi tatu ilikufikia malengo.

Alisema wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya kupambania timu ili kutafuta ushindi katika mchezo huo ingawa pia wanatambua Yanga Princess kwa sasa iko imara katika kila nafasi.

"Tunahitaji kurejesha heshima yetu, ili kufikia malengo yetu, lazima tupambane tushinde, tunawaheshimu Yanga Princess ambao wako vizuri, lakini kikubwa tunahitaji pointi tatu muhimu.

„Tutafanya mabadiliko makubwa ya kikosi ambacho kilicheza mechi ya kwanza ya Ngao ya Jamii, tunaingia kivingine na tumejipanga vizuri kwa msimu huu kufikia malengo yetu," alisema Mgosi.

Aliongeza kuwa mipango na mikakati yao itabaki kuwa siri ya benchi la ufundi, lakini kazi kubwa imefanyika kuandaa kikosi na kutarajia kupata ushindi.

"Kikubwa tunatafuta alama tatu iwe idadi ya mabao yoyote yale, wakiingia kwenye mfumo basi tutaweza kufunga mengi zaidi, mechi itakuwa nzuri na ya ufundi ndani ya uwanja," alisema kocha huyo.

Nahodha wa Simba Queens, Violeth Nicholas, alisema wamejiandaa vizuri na wako tayari kupambana kusaka alama tatu dhidi ya Yanga Princess.

Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Charles Haalubono, alisema wamejiandaa na anaimani utakuwa mchezo mzuri na wanahitaji matokeo mazuri mbele ya Simba Queens.

Alisema kila mchezo lazima uwe na presha hata unapocheza na timu ndogo inaweza kukupa mechi ngumu ila kikubwa ni jinsi ulivyojiandaa.

"Hatuna majeraha, mashabiki wajitokeze kusapoti, itakuwa mechi nzuri na ya ushindani kwa sababu ya kila mmoja kuhitaji matokeo mazuri ya alama tatu," alisema Haalubono.

KITAELEWEKA TU...



Wachezaji wa Taifa Stars, Ben Starkie (kushoto) na Simon Msuva, wakiwa Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Dar es Salaam juzi kwa safari ya Misri kwa ajili kambi ya wiki moja kabla ya kuelekea Ivory Coast kwenye Fainali za Mataifa ya Afrika, AFCON 2023. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# JKU yatoa sababu kichapo Mapinduzi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa timu ya Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU SC), Salum Ali Haji, amesema uzoefu wa wachezaji wa Simba ndio ambao umewaadhibu katika mchezo wao wa pili wa Kombe la Mapinduzi juzi.

Haji aliyasema hayo katika Uwanja wa Amaan Sports Complex baada ya mchezo wao uliomalizika kwa Simba kushinda mabao 3-1 juzi.

Alisema kupitia mchezo huo wamejifunza kitu na wanarudi kwa ajili ya kufanyia marekebisho makosa yote ambayo yamejitokeza kwenye mechi hiyo.

Alisema tatizo kikosi chake hakikuwa viuri katika kupambana na hawawezo kucheza muda wote.

Hata hivyo, alisema mpira ni mchezo wa makosa na makosa hayo wanakwenda kuyarekebisha na si kwa ajili ya Kombe la Mapinduzi tu bali pia kwa Ligi Kuu Zanzibar kwani mashindano hayo kwao ni sehemu ya mazoezi.

"Nadhani kwenye meza hii nilisema kwamba tukirudi tena hatutacheza kama ambavyo tulicheza mechi ya kwanza na vijana wameonesha mchezo mzuri tofauti na walivyocheza na Singida FG," alisema.

Katika mchezo huo mabao ya Simba yalifungwa Moses Phiri dakika ya nane, huku beki wa JKU, Mohamed Hassan akijifunga dakika ya 63 na Saleh Karabaka dakika ya 65. Bao la JKU

## Benchikha ataja gonjwa linalotesa

INATOKA UK. 24

Wakati kocha Benchikha akisema hayo, Kocha wa Singida Fountain Gate, Thabo Senong, amesema mchezo wa leo anauchukulia kwa uzito mkubwa kutokana na uwezo wa Simba.

Singida FG itaingia uwanjani leo huku tayari ikiwa na matumaini ya kusonga mbele kutokana na ushindi walioupata kwenye michezo miwili iliyopita dhidi ya JKU walishinda mabao 4-0 na kisha kuichapa APR 3-1 na kujikusanyia pointi sita.

Senog alisema utakuwa mchezo mgumu na wenye uhitaji wa kupata alama tatu kwa timu zote mbili na kwamba anawafahamu wapinzani wao hao kuwa wana wachezaji wazuri na wenye uwezo mkubwa, hivyo kwa upande wao kikubwa ni kuendeleza yale waliyafanya kwenye mechi mbili zilizopita.

Alisema yeye kama mwalimu kikubwa ni kuhakikisha anawajenga wachezaji wake kisaikolojia ili kutokuwa na hofu ya mchezo.

"Tunacheza na timu kubwa yenye uwezo na uzoefu katika soka, hivyo lazima tucheze kwa mipango ili kuhakikisha tunashinda mchezo huu ambao ni muhimu kwetu sisi, lazima wachezaji wawe na jitihada kubwa ingawa wanauchovu kulingana na ratiba yenyewe," alisema Senog.

Alisema watacheza kwa nidhamu kubwa kwenye mchezo wa leo ili kuhakikisha wanapata ushindi.

Kauli hiyo iliungwa mkono na nahodha wa timu hiyo, Gadiel Michael, ambaye alisema wanaiheshimu Simba kutokana na ukubwa wa timu hiyo, lakini watakuwa makini ili kuhakikisha wanamaliza hatua ya makundi wakiwa wameshinda michezo yao yote.

"Michezo yote ni migumu ambayo tumekutana nayo, lakini tumefanikiwa kushinda, hivyo matarajio yetu wachezaji ni kuona mchezo huu tunashinda na tutafanikiwa iwapo tutajituma kama ilivyokuwa mechi zilizopita," alisema Gadiel.

## Yanga yaweka wazi wachezaji

INATOKA UK. 24

ambalo lina uhaba wa wachezaji wengi bora walio huru.

„Kipindi hiki cha dirisha dogo ni mara chache sana kuweza kufanikisha kile ambacho unakitamani, kwa hiyo baada ya usajili wa wachezaji hawa wawili maingizo yaliyobaki si mengi, lakini halitopungua moja," alisema.

Yanga inahusishwa kumsajili straika Leonel Ateba kutoka Klabu ya Dynamo FC de Douala ya Cameroon ambaye kwa sasa yupo na kikosi cha timu ya taifa ya nchi hiyo, inayotarajiwa kucheza michuano ya AFCON nchini Ivory Coast.

Kwa sasa timu hiyo inaongoza kwenye Ligi Kuu nchini humo ikiwa Kundi A na pointi 24 kwa mechi 13 ilizocheza na haikushiriki michuano yoyote ya kimataifa msimu huu.

Michezo

Salah anogesha mbio kiatu cha Dhahabu EPL UKURASA 21

Jumatano Januari 3, 2024

Nipashe





# BENCHIKHA SASA ATAJA GONJWA LINALOTESA MABEKI SIMBA

●●● Ni wakati wakiivaa Singida FG Mapinduzi leo, akunwa na Karabaka, asema...

Kiungo wa Simba, Fabrice Ngoma (kushoto), akimpongeza winga wa timu hiyo, Saleh Karabaka, baada ya kufunga bao la tatu wakati wakishinda 3-1 dhidi ya JKU kwenye mechi ya Kombe la Mapinduzi iliyopigwa Uwanja wa Amaan Sports Complex, Zanzibar juzi usiku. **MPIGAPICHA WETU**

**Faustine Feliciane na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKATI leo ikishuka tena Uwanja wa Amaan Sports Complex, kucheza mchezo wake wa pili wa michuano ya Kombe la Mapinduzi, Kocha wa Simba, Abdelhak Benchikha, amesema bado safu yake ya ulinzi ina shida kutokana na kuruhusu magoli kirahisi, huku akibainisha ‚gonjwa' linalowasumbua.

Simba ambayo juzi iliibuka na ushindi wa mabao 3-1 katika mchezo wake wa kwanza wa michuano hiyo dhidi ya JKU SC na leo saa 2:15 usiku itavaana na Singida Fountain Gate ambayo nayo siku hiyo ilipata ushindi kama huo dhidi ya APR ya Rwanda.

Akizungumza na Nipashe jana, Benchikha alisema amebaini tatizo kubwa la mabeki wake wanacheza kwa kujiamini kupitiliza jambo ambalo mara nyingine husababisha makosa yanayowagharimu.

„Jambo jema tulipata ushindi katika mchezo wetu wa kwanza, lakini kuna makosa ambayo niliyaona hasa safu yangu ya ulinzi, tumekuwa tukiruhusu magoli mepesi sana, tatizo ni mabeki kucheza kwa kujiamini sana na kusababisha kufanya makosa yanayotugharimu, nimewaambia lazima wabadilike...mchezo wa leo hatupaswi kufanya makosa kama tulivyofanya na JKU,“ alisema Benchikha.

Aidha, alisema michuano hiyo ya Mapinduzi imeifurahia kwa kuwa inampa nafasi ya kukiimarisha kikosi chake na kuweza kuwatumia vema wachezaji ambao hawajapata nafasi kubwa kwenye michezo ya Ligi Kuu.

„Kuna wachezaji nafurahia kile wanachokionesha, haya mashindano yatanipa wigo mpana wa kuwaona wachezaji wangu na kuwapa vitu vitakavyotuimarisha zaidi,“ alisema Benchikha.

Alisema mchezaji kama Saleh Karabaka ameonesha uwezo mkubwa na muda mfupi alioingia uwanjani kwenye mchezo dhidi ya JKU alifanikiwa kufunga bao katika ushindi wa mabao 3-1 juzi.

“Nimefurahi kuona kati ya magoli matatu yaliyofungwa moja ni la kwake, Karabaka ni mchezaji kijana lakini ana malengo ya kufika mbali,” alisema.

Hata hivyo, alisema ni imani yake kwamba mchezaji huyo ataonesha kiwango zaidi na zaidi kama ambavyo wachezaji wenzake wengine wanaosajiliwa kutoka visiwani wanavyokuwa.

“Tumemsjaili na kwa mechi hii namuona yupo vizuri na matumaini yangu kiwango chake kitazidi kukua kila baada ya muda pale atakapopata mechi nyingi,” alisema.

INAENDELEA UK. 23

# Yanga yaanika wachezaji itakaowasajili

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema imebakiza nafasi mbili za usajili, ikiweka wazi aina ya wachezaji itakaowasajili kuwa ni wale tu ambao hawajacheza mechi zozote za kimataifa wakiwa na timu zao msimu huu.

Makamu wa rais wa klabu hiyo, Arafat Haji (pichani), amesema jana kuwa, zipo tetesi nyingi zikiihusisha Yanga kusajili wachezaji mbalimbali wakiwamo wa timu za Medeama ya Ghana, Jwaneng Galaxy ya Botswana na Asec Mimosas ya Ivory Coast, lakini ukweli ni kwamba watasajili wachezaji ambao timu zao hazikucheza michuano hiyo ili wakishasajiliwa wasibanwe kucheza michuano hiyo.



„Tunataka wachezaji ambao tukiwasajili waingie moja kwa moja kuisaidia timu kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa, wachezaji wa timu hizo hata kama tukiwasajili hawatocheza kwa hiyo hakuna faida yoyote.

„Malengo yetu kwenye kikosi ni kupata wachezaji ambao wataingia moja kwa moja kwenye kikosi na kucheza michuano ya kimataifa, kwa hiyo yeyote ambaye atasajiliwa basi ni yule ambaye hajacheza kabisa michuano hiyo.

Nani anaingia watu wameanza kuona, tumeanza kwa kumsajili Shekhan Ibrahim Khamis na wa pili ni Augustine Okrah, lakini nani anatoka bado tutakuja baadaye kuwaeleza Wananga,“ alisema Arafat.

Alisema kwa sasa wanaendelea kuifanyia kazi ripoti ya Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, ambaye amewaambia kuwe na maingizo ya wachezaji wachache, hasa kwenye dirisha dogo

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >